



# **VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

## **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

## **SURA YA KWANZA**

### **JE! KANISA NI NINI?**

**MASOMO YA BIBLIA:** I Wakorintho 12:12-13, 20-27; Mathayo 16:15-18

Siku moja, Tom alikutana na rafiki yake Danieli akiwa anatembea barabarani.

**Tom:** "Habari yako."

**Danieli:** "Njema sana, Tom. Je! ulikuwa wapi?"

**Tom:** "Nilikuwa kanisani."

**Danieli:** "Je! kanisa lako liko wapi?"

**Tom:** "Liko huko chini karibu na mto. Nadhani hivi karibuni tutakuja kwenda sote na kuhudhuria huko."

**Danieli:** "Je! kanisa lako limejengwa na nini?"

**Tom:** "Limejengwa na mbao na kuezekwa na mabati."

**Danieli:** "Je! kanisa hilo lina vyumba vingapi?"

**Tom:** "Ngoja kidogo. Nafikiri lina vyumba vinne."

**Danieli:** "Je! ni jengo zuri?"


**Tom:** "Ndiyo, nadhani ni zuri. Hata sijafikiria juu ya jambo hili."

**Danieli:** "Tom, unanitaka nije kanisani kwenu, hali hujui jinsi jengo hilo lilivyo!"

**Tom:** "Danieli, kanisa letu si jengo tu, kanisa letu ni kundi la watu ambao wanamwabudu na kumtumikia Mungu."

### **KANISA NI WATU**

Watu wengi ni kama Danieli. Hufikiria kuwa kanisa ni jengo bali sio watu. Wao husema kwamba, "Kanisa langu limejengwa na mawe na lina vyumba vinne. Lina mlango, madirisha na limezekwa na mabati." Wao huwasahau watu mbalimbali ambao ndio kanisa.



Hata hawajui kwamba wale watu wanaokutanika katika jengo hilo kwa kumwabudu Mungu na kumtumikia ndio kanisa.



## KANISA NI MWILI MMOJA

Wakorintho wa Kwanza 12:20-27 inatufundisha kwamba sisi ni kitu kimoja. Hii inamaanisha kwamba tu sehemu ya kundi moja. Sisi tu mwili mmoja kwa sababu tunamtumikia Mungu. Vifungu hivi vinatuambia kwamba watu wengi wa aina mbali mbali hulifanya kanisa lake. Watu hawa wote wanatakikana katika kanisa. Watu hawa mbalimbali ni kama viungo tofauti vya mwili.

Tunahitaji viungo vyote vya miili yetu. Hatungeweza kutembea iwapo hatungekuwa na miguu, wala hatungeweza kuongea bila kuwa na

mdomo. Tumbo zetu hubadili chakula tulacho ili miili yetu iwe na nguvu na afya nzuri hata tuweze kupata nguvu zaidi. Hatungeweza kusikia ndege wakiimba bila kuwa na masikio, au wazazi wetu watwitapo. Pia, hatungeweza kuona vitu vyote vilivyo-umbwa na Mungu bila kuwa na macho. Mungu alitupa viungo hivi tofauti vya miili yetu kwa sababu alijua kwamba tunavihitaji.

## NI LAZIMA WASHIRIKI WA KANISA WAFANYE KAZI PAMOJA

Kanisa huhitaji na hutumia watu mbalimbali ambao humtumikia Mungu, jinsi sisi nasi tunavyohitaji na kutumia viungo mbalimbali vya miili yetu.

Je! Kanisa lingefanya nini bila kuwa na mchungaji, kiongozi wa nyimbo, mashemasi, na waalimu wa Shule ya Jumapili? Watu hawa huwaongoza wengine katika kumtukuza Mungu na kujifunza Neno la Mungu na kujifunza mengi kuhusu Mungu, na jinsi ya kumtumikia.

Mungu huhitaji tu viongozi wa kanisa. Anahitaji kila mmoja wetu amfanyie kazi. Kila mmoja wetu anaweza kufanya kitu fulani.

Yohana ni mwimbaji mzuri. Wakati mwingine huwa anaimba nyimbo maalum wakati wa Jumapili. Maria ni msomaji mzuri. Yeye huwasomea watoto wadogo Biblia wakati wa Shule ya Jumapili na kwa akina mama wazee ambao hawawezi kusoma. Paulo anapenda kuongea na watu, kwa hivyo, huwa anaenda na mchungaji kutembelea watu vijijini mwao.

Kuna kazi nyingi ambazo wavulana na wasichana wanaweza kufanya ili wasaidie kanisa—kuchukua sadaka, kufagia na kupamba kanisa, kuokota takataka zilizoko karibu na kanisa, kumpelekea mgonjwa maua au chakula, kuwaalika wengine kuja kanisani, kuwatunza watoto wakati wazazi wao hawapo au wanapohudhuria mikutano ya kanisa.

Mungu anatumia kazi tumfanyie kazi na tuwaambie wenzetu na kuwaonyesha kwamba Mungu anawapenda, nasi pia tunawapenda.

Ni lazima watu wafanye kazi pamoja ili kanisa liweze kukua. Mtu hawezi kujenga nyumba akiwa peke yake. Lakini anaweza kujenga nyumba hiyo iwapo atasaidia na watu wengine. Watu wanaweza kufanya kazi kubwa iwapo watashirikiana pamoja.

Mungu alimwambia Simoni Petro katika Mathayo 16:18 kwamba hakutakuwa na cho chote ambacho kitaweza kuangamiza kanisa lake. Jengo la kanisa linaweza kuungua kwa moto au kuharibiwa na mafuriko au dhoruba, lakini hakuna kiwezacho kuharibu kundi la Wakristo ambao ni kanisa. Roho za watu hawa haziwezi kuharibiwa hata ingawa wanaweza kuuawa, kwa sababu Mungu yu pamoja nao.

## KAZI YA KUFANYA

Weka alama ya (✓) kando ya jibu sahihi.

Kanisa ni

—jengo tu.

—kundi la watu ambao wanamwabudu na kumtumikia Mungu.

—hufunguliwa tu wakati wa Jumapili.

Mungu anawataka na anawatarajia watu wa umti wote kumsaidia katika kanisa. Piga msitari chini ya yale uwezayo kufanya ili umsaidie Mungu.

Nile mahindi jinsi niwezavyo. Nimsomee Biblia mtu ambaye hawezi kusoma. Nimpelekee mgonjwa chakula. Nimchokoze dada au ndugu yangu mdogo. Nikusanye sadaka. Nipande maua kuzunguka kanisa.

Chora mviringo kwa vitu ambavyo ni vya kanisa.

Mbwa, gari, Biblia, mhubiri, pesa, watu

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo.

1. "Kwa maana katika \_\_\_\_\_ sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja..." (1 Wakorintho 12:13a).

2. Kanisa ni \_\_\_\_\_.
3. "Lakini sasa viungo ni vingi, ila \_\_\_\_\_ ni \_\_\_\_\_." (1 Wakorintho 12:20)
4. Yule anayezungumza katika Mathayo 16:16 ni \_\_\_\_\_.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"...Kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25b).

Yesu alilipenda sana kanisa hata akafa kwa ajili yake. Hakutoa uhai wake kwa ajili ya jengo lakini kwa ajili ya watu ambao wanamwamini, na kumwabudu na kumtumikia.

Tunapaswa kupenda kanisa jinsi Yesu alivyolipenda. Tunapaswa pia kuonyesha kwamba tunalipenda kanisa kwa kufanya kazi kanisani. Mungu anawataka na anawahitaji watu wa kila umri wamtumikie katika kanisa lake.




**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**  
**MWAKA WA TATU KITABU CHA TATU**  
**TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**  
**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

**SURA YA PILI**  
**JE! KANISA LIMEKUWAJE?**

**MASOMO YA BIBLIA:** Mathayo  
28:18-20; Matendo 8:1-4

Hebu leo tujifanye kama kwamba  
tunasikiliza kipindi cha redio.



**Msimulizi:** “Nawashukuru nyote  
mnaosikiliza kipindi hiki katika redio  
zenu. Leo tutazungumzia wamisheni  
wakuu walioishi tangu zamani.

Mmisheni ni yule ambaye  
anawaambia wengine habari za Yesu.

“Wamisheni wanaweza ku-  
mwendea jirani kumwambia habari  
za Mungu. Au wanaweza kwenda  
kwa kijiji jirani au nchi nyingine  
kama wamisheni. Wanaweza pia  
wakazunguka ulimwenguni kote  
wakishiriki habari za Mungu na  
wenzao.

“Yesu aliwatuma wamisheni wa  
kwanza kabla ya kwenda mbinguni  
kuwa na Mungu. Wamisheni wa  
kwanza walikuwa wanafunzi wake.  
Yesu aliwaambia kwamba ata-  
watumia Roho Mtakatifu ili  
awasaidie na kuwapa nguvu za  
kuweza kuwaambia wenzao habari  
za Yesu. Akawaambia, “...nanyi  
mtakuwa mashahidi wangu katika  
Yerusalemu, na katika Uyahudi  
wote, na Samaria, na hata mwisho wa  
nchi.” (Matendo 1:8b). Kisha  
akachukuliwa kwenda juu mbinguni  
kuwa pamoja na Mungu.

“Yesu alipoenda mbinguni aliwatarajia wafuasi wake kuendelea na kazi yake. Wote walipaswa kuwaambia wengine jinsi Mungu alivyowapenda sana hata akamtuma Yesu kufa kwa ajili ya dhambi zao. Roho Mtakatifu aliwapa wamisheni hawa nguvu za kuweza kushiriki injili na wenzao.

“Naweza kumwona mtu mmoja akija. Hebu tuongee naye. Tafadhali Bwana. Je! wewe ni mmisheni?”

**Paulo:** “Ndiyo. Jina langu ni Paulo. Sikuwa nikiitwa Paulo. Hapo awali nilikuwa nikiitwa Saulo. Nami sikuwa Mkristo wakati huo. Niliwachukia sana Wakristo kwa sababu walimfuata Mungu. Niliwashika na nikawafunga gerezani wanaume na wanawake wengi. Halafu siku moja nikawa naelekea Dameski. Mara kwa ghafula nikaangaziwa na nuru kuu ambayo iliniangusha chini. Nikawa kipofu.



Hatimaye nikasikia sauti ikiniambia, “Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe.” Sikutaka tena kuwasumbua Wakristo. Sasa nilimhitaji mtu wa kuniongoza hadi mjini kwa sababu nilikuwa kipofu.

“Hatimaye nilisaidiwa na Wakristo wengine nami nikawa mmisheni. Sasa, badala ya kuwasumbua wale waliomwamini Mungu, nawasaidia na kuwaambia habari za Mungu. Roho Mtakatifu alinisaidia na akanijaza na nguvu.”

**Msimulizi:** “Naweza kumwona pia mtu mwingine akija. Hujambo Bwana! Je! wewe ni nani?”

**Filipo:** “Jina langu ni Filipino. Nilipatwa na jambo la ajabu sana kutoka kwa Bwana ambalo ningependa kuwaambia. Malaika wa Bwana alinitokezea siku moja na akaniambia niende hadi kwa njia itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza. Sikujua ni kwa nini lakini nilienda. Halafu nikakutana na mtu mmoja wa Ethiopia (Kushi), nchi mojawapo ya Afrika. Alikuwa afisa mkuu katika serikali. Alikuwa na hati ya kuviringisha. Naye alikuwa akisoma Maandiko, lakini hakuwa akiyaelewa.

“Roho Mtakatifu aliniongoza kumwendea yule mkushi na kumwuliza iwapo naweza kumwelezea Maandiko yale. Mtu huyo alifurahi sana. Alitamani kuelewa maana ya Maandiko yale.

“Nilimwelezea maana ya yale aliyokuwa akisoma kutoka kwa nabii Isaya. Nilimwambia habari njema ya Yesu, na jinsi ya kuwa Mkristo. Hatimaye tulifika karibu na maji ya mto nami nikambatiza. Sote tulifurahi sana siku hiyo. Roho Mtakatifu ndiye aliyemwezesha kushiriki habari za Mungu na wengine.”



nyingi nilipokuwa mgonjwa au mwenye huzuni. Siku moja nilipigana na simba, lakini Mungu aliweza kunilinda. Alikuwa pia pamoja nami nilipougua ugonjwa wa malaria na wakati mke wangu alipokufa kwa ajili ya malaria. Ningekata tamaa kwa urahisi iwapo hakungekuwa na Mungu na Roho yake Mtakatifu.”

**Msimulizi:** “Tumeshasikiliza wamisheni wakuu watatu ambao wameshiriki habari za Mungu tangu hapo zamani. Mungu alitumia Roho Mtakatifu kuwasaidia watu hawa na kuwa pamoja nao. Je! utakuwa leo mmisheni wa Mungu? Je! utamwambia mtu mwingine yale ambayo Mungu amekufanyia? Alimtuma Mwanawe wa pekee, Yesu, ili kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako.


**Msimulizi:** “Naweza kumwona tena mtu mwingine akija. Je! wewe ni nani? Tena hafanani na wale wamisheni wawili ambao nimesha wahoji.

**David Livingstone:** “Jina langu ni David Livingstone. Sikuishi wakati wa mwanzo wa Biblia. Nilizaliwa mwaka wa 1813 kule Scotland. Niliamua kuwa mmisheni wakati nilipokuwa mkubwa. Kwanza nilisomea Udaktari. Baada ya kupata kuwa daktari niliamua kwenda Afrika. Nilipofika Afrika kwa mara ya kwanza nilikuwa nikiishi mahali paitwapo Cape Town. Halafu nikaanza kutembelea sehemu mbalimbali za Afrika nikiwatibu wagonjwa, na kuwaambia habari za Mungu. Roho Mtakatifu alinisaidia sana mara

“Kipindi hiki cha redio kimekusaidia kuweza kufahamu jinsi kanisa lilivyokua. Yesu aliporudi mbinguni aliwaacha watu kumi na wawili kufanya kazi yake. Roho Mtakatifu aliwasaidia watu hawa kuhubiri injili na hata watu wengi kumfahamu Yesu Kristo. Mmisheni aitwaye Paulo na wengine waliipeleka Injili hadi Asia ambako pia ilienezwa katika nchi ya Ulaya. Siku hizi kuna makanisa mengi ulimwenguni kote hata ingawa kanisa lilianza na kundi dogo la waamini. Hii ni kwa sababu ya wamisheni ambao walitoka sehemu mbalimbali za ulimwengu ili kushiriki ujumbe wa Mungu na watu ambao hawajawahi kusikia kuhusu nguvu za ukombozi wa Mungu.”

## KAZI YA KUFANYA

Unganisha namba zifuatazo, kuanzia 1 hadi 2 hadi 3 na kadhalika mpaka 24 kwa kuchora mstari ili uone kile kitu ambacho Mwethiopia alikuwa akisoma wakati Filipo alipomwona.



Sentensi mbili kati ya hizi zifuatazo ni za kweli na moja si ya kweli. Weka alama (✓) kando ya zile zilizo za kweli na ukate kwa mstari sentensi ile ambayo si ya kweli.

\_\_\_\_ Paulo alikuwa akiitwa zamani Saulo.

\_\_\_\_ Paulo aliwapenda Wakristo.

\_\_\_\_ Paulo alipofuka alipokuwa njiani akielekea Dameski.

Uliwasikia wamisheni watatu wakizungumza katika kipindi cha redio. Andika majina ya wale wawili ambao waliwaelezea watu wa Afrika habari za injili.

1. \_\_\_\_\_

2. \_\_\_\_\_

Weka alama ya (✓) kando ya jibu lililo sahihi.

Mmisheni ni:

\_\_\_\_mwuzaji wa samaki.

\_\_\_\_yule anayewaambia wengine habari za Mungu.

\_\_\_\_yule anayewatukana Wakristo.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8).

Mungu alifahamu udhaifu wetu. Alijua kwamba hatungeweza kushuhudia bila usaidizi wake. Kwa hivyo, alimtuma Roho Mtakatifu kuwa pamoja nasi na kutusaidia. Roho Mtakatifu ataenda pamoja nasi po pote tuendapo hapa ulimwenguni tunapowaambia wengine juu ya upendo wa Mungu.



# **VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA**

## **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

## **SURA YA TATU**

### **UJUMBE MKUU WA KANISA**

**MASOMO YA BIBLIA:** Matendo  
4:5-12

Petro na Yohana walikuwa wamefanya kitendo chema. Walikuwa wamemponya kiwete. Walishikwa walipofanya kitendo hiki na kupelekwa kwa baraza la hukumu kule Yerusalemu. Hebu tujifanye kwamba tuko huko na tunasikiliza yale ambayo yanasemwa.



**MCHEZO WA KUIGIZA**

(Mahali: Katika Korti ya Yerusalemu)

**Anasi:** “Mmeshtakiwa leo kwa sababu mmeponya kiwete mmoja. Alikuwa kiwete na sasa anatembea. Hamwezi kukana shtaka hili kwa sababu kila mmoja amemwona akitembea. Je! mliwezaje kumponya? Mmeshtakiwa pia kwa kufundisha kwamba mtu aitwaye Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Je! mtu aliyekufa anaweza kufufuka?”

**Kayafa:** “Ninyi mmetukasirisha sana kwa kuwafundisha watu wetu. Ha’ukubaliani na yale ambayo mnafanya na tunataka mwache.”

**Iskanda:** “Hebu tuambieni. Mwasemaje juu ya mashtaka haya? Semenii!

**Petro:** (Anaomba) “Oh, Bwana, tafadhali nakuomba unisaidie. Nipe maneno mema ya kuwaambia watu hawa ili jina lako litukuzwe.” (Anawageukia watu wale) “Mnataka mjue kwa nini kiwete yule ameweza kutembea. Aliponywa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti.”



**Anasi:** "Yesu Kristo? Unamaanisha yule mtu aliuawa msalabani kwa kujilinganisha kuwa sawa na Mungu? Je! kwa nini uliponya kwa jina lake?"

**Petro:** "Inaonekana wazi kwamba ninyi hamwelewi Yesu alikuwa nani. Yeye ni Mwana pekee wa Mungu. Alikuwa ulimwenguni ili kuishi pamoja nasi. Alifanya matendo mengi mema ili kutusaidia. Hata hivyo, alisulibiwa tu msalabani. Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Nasi tunamwamini Yesu Kristo. Yeye ndiye Mwokozi wetu wa pekee. Hii inamaanisha kwamba alikufa ili atuokoe kutoka dhambini. Tunaweza tu kuokolewa kupitia kwake. Hakuna jina lingine hapa duniani wala mbinguni ambalo tunaweza kuokolewa kwalo. Yesu pia ni Bwana wa maisha yetu. Hii inamaanisha kwamba yeye anatusaidia katika yote tufanyayo, na hutuonyesha kile ambacho tunapaswa kufanya. Sisi ni Wakristo kwa sababu tulimpokea Kristo kama Mwokozi wetu."

(Mwisho)

## USHUHUDA WA PETRO

Wale watu waliokuwa katika korti walimsikiliza tu Petro. Walitaka kusikia yale ambayo angesema. Walijua kwamba Mungu alikuwa pamoja naye. Petro hangeweza kusema haya yote kwa uwezo wake. Mungu alimsaidia.

Petro aliwaambia watu hao kwamba wanaweza kuwa Wakristo. Aliwaambia kwamba njia pekee ya kuwa Mkristo ni kuamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Alisema pia kwamba ni lazima waamini kuwa alifia dhambi zetu, na akafufuka kutoka kaburini.

Petro aliamini mambo haya yahusuyo Yesu. Hakutegemea nguvu zake mwenyewe kwa kutenda kazi, wala hekima yake kwa kusema yale aliyosema. Roho Mtakatifu wa Mungu ndiye aliyekuwa chanzo cha ujasiri wake. Jambo hili lilimwezesha kulitukuza jina la Mungu mbele ya watu hawa. Petro alifuata mafundisho ya Yesu na akajaribu kuwa kama Yesu.

## YESU NI KICHWA CHA KANISA

Kanisa linatufundisha kumwamini Yesu. Yeye ni kichwa cha kanisa. Yeye ndiye msingi wa kanisa. Hii inamaanisha kwamba kanisa linamfuata Yesu na mafundisho yake.

Washiriki wa kanisa huwaambia wengine habari za Yesu. Huwaacha wengine wamwone Yesu kwa yale watendayo na yale wasemayo. Yule ambaye huwaambia wengine habari za Yesu lakini hatendi mema huwa hamsaidi Yesu.

Je! wewe ukoje? Je! umekwisha kumpokea Yesu kama Mwokozi wa maisha yako? Ikiwa bado, Je! ungependa kumpokea sasa hivi? Mwombe akusamehe dhambi zako na awe Bwana wako.

Kama wewe u Mkristo, Je! wenzako wanajua hivyo kutokana na maisha yako? Je! unaujasiri kama Petro? Je! unawaonyesha wengine njia ya kumfikia Yesu? Tumia dakika chache sasa ili ufikirie majibu yako kwa maswali haya.

### KAZI YA KUFANYA

Piga mstari chini ya sentensi za kweli zihusuzo Petro.

Petro alimponya kiwete yule ili aweze kujulikana sana.

Aliogopa kuwaambia wazee, wakubwa na waandishi wa kiyahudi habari za Yesu.


Petro alimtegemea Yesu kwa kumpa uwezo wa kumwezesha kuhubiri na kuponya.

Alisema kwamba wokovu unapatikana kwa Yesu pekee.

Petro alihubiri kwamba Yesu ndiye jiwe pekee la pembeni la kanisa.

Chora mviringo juu ya jibu lililo sahihi.

Petro alimponya kiwete yule katika jina la:



Yesu



Kanisa



Mfalme

Je! ni nani kichwa cha kanisa? Weka alama (✓) kando ya jibu lililo sahihi.

\_\_\_ Wanafunzi kumi na wawili.

\_\_\_ Mchungaji wangu.

\_\_\_ Yesu Kristo.

\_\_\_ Washiriki wa kanisa.

**Andika katika nafasi ifuatayo yale ulewayo kuwa ndiyo ujumbe wa kanisa (Tazama Matendo 4:11-12.)**

---

---

---

**Ikiwa wewe ni Mkristo na mshiriki wa kanisa, taja njia ambazo unaweza kushiriki ujumbe huu na wenzako.**

---

---

---

---

**Ikiwa Petro alikuwa anataka kufanya hivyo, basi angewaambia wale waliokuwa kortini mambo mengi yahusuyo kanisa. Hata hivyo, aliwaambia yale yaliyo ya muhimu tu. Aliwaambia habari ya Yesu. Petro aliwaeleza kuwa Yesu ni nani na yale aliyofanya.**

**Tunaweza kuwaambia watu mambo mengi yahusuyo kanisa. Hili ni jambo jema, lakini halitoshi. Tutakuwa tunaacha ujumbe muhimu wa kanisa iwapo hatuwaambii wenzetu habari za Yesu. Yesu ndiye jiwe la pembeni ambalo kanisa limejengwa juu yake. Ikiwa hatuwaambii watu habari zake, basi hatuwaambii kuhusu kanisa.**

#### **KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**“Wala hakuna wokovu katika mwingine, awaye yote, kwa maana hapa jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Matendo 4:12).**



**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**  
**MWAKA WA TATU KITABU CHA TATU**  
**TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

**SURA YA NNE**

**JE! Naweza kuwa mshiriki wa kanisa?**

**MASOMO YA BIBLIA:** Matendo  
2:36-42

Siku moja asuhubi baada ya Shule ya Jumapili, Anna alitaka kusema na mwalimu wake. Rafiki zake walikuwa washiriki wa kanisa naye alimtaka mwalimu wake amsaidie ili awe mshiriki. Hebu tusikilize kwa makini wakati wanapojadiliana.



**Anna:** "Tafadhali mwalimu, nataka niwe mshiriki wa kanisa hili."

**Mwalimu:** "Hivyo ni vizuri sana, Anna. Je! kwa nini unataka uwe mshiriki wa kanisa?"

**Anna:** "Nataka niwe mshiriki kwa sababu marafiki zangu wote ni washiriki wa kanisa hili. Nataka niwe mmoja wao."

**Mwalimu:** "Anna, nafikiri huelewi maana ya kuwa mshiriki wa kanisa."

**Anna:** "Je! mwalimu, inamaanisha nini?"

**Mwalimu:** "Anna, ni lazima ufanye jambo moja muhimu kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa."

**Anna:** "Je! ninapaswa nifanye nini? Sikujua ninapaswa kufanya jambo lingine kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa."

**Mwalimu:** “Ndiyo, ni lazima utubu dhambi zako na umpokee Yesu Kristo kama Mwokozi wako kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa.

**Anna:** “Je! nitafanyaje hivyo? Je! unamaanisha unaposema nitubu na kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wangu?”

**Mwalimu:** “Kutubu kunamaanisha kuacha na kubadili mwenendo wako. Mtu ambaye si Mkristo hufuata mapenzi yake. Lakini anapobadili na kumfuata Yesu, hutaka kujuana kufanya mapenzi ya Mungu. Ikiwa unamfuata Yesu ni lazima uamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu. Ni lazima uamini kwamba Yesu alikupenda sana hata akafa ili akuokoe kutoka dhambini na kwamba alifufuka kutoka kwa wafu.”

**Anna:** “Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zangu? Lakini sijawahi kutenda dhambi nyingi.”

**Mwalimu:** “Biblia inatuambia kwamba kila mmoja wetu amefanya dhambi. Warumi 3:23 inasema kwamba, wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Dhambi hututenganisha na Mungu. Dhambi ni kama ukuta ambao uko kati yetu na Mungu. Mwenye dhambi hawezi kufanya chochote ili abomoe ukuta huu. Yesu aliondoa ukuta huu alipotufia. Ni lazima uwe na imani ili uamini kwamba alikufanyia hivyo.”

**Anna:** “Je! ni nini kitakachofanyika baada ya kumpokea Yesu kama Mwokozi wangu?”

**Mwalimu:** “Ni lazima umwombe Yesu awe Bwana wa maisha yako.”

**Anna:** “Bwana wa maisha yangu? Hiyo inaonekana kama mimi ni mtumwa. Je! nitakuwa mtumwa?”

**Mwalimu:** “La, hutakuwa mtumwa. Pengine utafikiria hivyo, lakini utakuwa huru iwapo utampokea Yesu. Yesu anataka kuongoza maisha yako. Anataka kuwa pamoja nawe. Anakutaka umwulize jambo la kufanya na kusema. Unaweza kumwomba na kumwuliza akuongoze.”

**Anna:** “Dada yangu alipata kuwa Mkristo mwaka uliopita. Mimi humsikia akiomba na kuzungumza na Yesu wakati wa asubuhi ninapojitayarisha kwenda shuleni. Husoma sana Biblia.”

**Mwalimu:** “Anna, hivyo ni vizuri. Kuomba na kusoma Biblia ni mambo muhimu kwa Mkristo. Hivyo ndivyo Mungu anavyosema nasi na jinsi tunavyosema naye.”

**Anna:** “Tafadhali niambie. Ni nini kitakachofanyika baada ya nimepata kuwa Mkristo. Je! wakati huo nitakuwa mshiriki wa kanisa?”

**Mwalimu:** “Kwanza ni lazima uliambie kanisa kwamba unataka uwe mshiriki. Halafu ubatizwe.”

**Anna:** “Nibatizwe? Je! kubatizwa ni nini? Je! kutaniumiza?”

**Mwalimu:** (Anacheke) “La, hakutakuumiza. Mchungaji atakupeleka mtoni. Halafu atakuingiza majini ili mwili wako

wote uwe majini. Halafu atakuinua juu na kukutoa humo."

**Anna:** "Je! unahakika kwamba sitatos majini?"

**Mwalimu:** "Hutatos majini!"

**Anna:** "Je! kwa nini nibatizwe mtoni?"

**Mwalimu:** "Si lazima ubatizwe tu mtoni. Unaweza kubatizwa mahali po pote ambapo pana maji ya kutosha ambayo mwili wako unaweza kuchovwa ndani—katika bahari, ziwa au kidimbwi."

**Anna:** "Je! kwa nini ni lazima nibatizwe?"

**Mwalimu:** "Yesu alibatizwa wakati alipoanza kufundisha na kuhubiri. Alifanya hivyo kama mfano kwetu. Ubatizo unamaanisha kwamba tumefia dhambi zetu na kuzaliwa upya kiroho. Yesu hakuwa na dhambi maishani mwake. Tunapompokea Yesu huwa tunapewa maisha mapya. Yesu hakuwa na dhambi maishani mwake. Alikuwa mkamilifu, lakini alibatizwa ili kutuonyesha kile tupaswacho kufanya. Tunapobatizwa huwa tunauonyesha ulimwengu kwamba tunamfuata Yesu."

**Anna:** "Je! ubatizo huwaokoa watu?"

**Mwalimu:** "La, ubatizo hauokoi. Huonyesha tu kwamba mtu huyo amemwamini Yesu. Ubatizo pia ni kama kufa na kufufuka kwa Yesu. Tuingiapo katika maji ni kama kifo cha Yesu, na tuinuliwapo kutoka majini ni kama kufufuka kwake."

**Anna:** "Asante sana mwalimu, kwa kunielezea jinsi niwezavyo kuwa mshiriki wa kanisa."

Soma vifungu vya Biblia vya somo la leo (Matendo 2:36-42). Mtu yule anayezungumza ni Petro. Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kuwapa watu wake nguvu za kuweza kuwaambia wengine habari za Yesu. Petro alianza kuhubiri kwamba Yesu ndiye Masihi, Mwokozi wa pekee. Mahubiri ya Petro yalianzia katika kifungu cha 14. Vifungu mliyosoma vina sehemu ya mwisho ya mahubiri yake. Vinatwambia pia jibu la Petro kwa watu wale waliotaka kujua jinsi ya kuokolewa.

Petro aliwaambia kwamba ni lazima watubu na wabatizwe. Hebu yatizame tena majadiliano kati ya Anna na mwalimu wake. Tafuta maana ya neno hili "kutubu". Je! Petro alimaanisha nini aliposema kwamba, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu?"

Alimaanisha kwamba ni lazima mtu abadili mwenendo wake wa maisha. Halafu abatizwe baada ya kutubu. Mtu habatizwi ili asamehewe dhambi zake. Bali hubatizwa kwa sababu amesamehewa tayari dhambi zake. Yeye husamehewa wakati anapotubu. Halafu baada ya kubatizwa huwa tayari kuwa mshiriki wa kanisa.

Watu wapatao elfu tatu wali-ongezeka kwa kanisa wakati Petro alipohubiri. Hata leo hii watu wapate kuwa washiriki wa kanisa jinsi walivyofanya wakati wa kanisa la mwanzo.

## KAZI YA KUFANYA

Piga mstari katika sentensi ambayo si ya kweli.\*

Ubatizo ndiyo njia ya kuwa Mkristo.

Ubatizo huwaonyeshe wengine kwamba umetubu dhambi zako na unataka kumfuata Yesu.

Mtu huwa Mkristo kabla ya kubatizwa.

Andika vizuḡi maneno yafuatayo ili utambue kile ambacho hutokea maishani mwa mtu kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa.

IN MAZILA ATUUB DHIMBA  
KAEZ AN MIMWANIA SUYE IIL  
AKOLOWEW

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo na viungo kila kimoja peke yake” (1 Wakorintho 12:27).

Ni lazima mtu ampokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wake kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa. Mtu huyo atakapomkiri Kristo, baadaye hutaka kuwa mshiriki wa kanisa na pia kubatizwa.

Kujiunga na kanisa au kubatizwa hakuwezi kumwokoā mtu kutoka kwa dhambi zake. Ni imani tu katika Yesu kama Mwokozi ambayo inaweza kumwokoā. Je! umempokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako? Ikiwa bado, Je! unaweza kufanya hivyo sasa hivi?

Je! Petro alisema kwamba wale wanaotubu watapokea nini? (Matendo 2:38b)

\_\_\_\_\_ cha \_\_\_\_\_

Chora katika nafasi ifuatayo picha ya mtu anayetuliza kuwa mshiriki wa kanisa au mtu anayebatizwa. Au, tafuta picha yo yote katika gazeti ihusuyo mtu anayetuliza kuwa mshiriki wa kanisa au mtu anayebatizwa. Shikamanisha picha hiyo katika nafasi ifuatayo.



# **VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

## **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

## **SURA YA TANO**

### **JE! UBATIZO UNAMAANISHA NINI?**

**MASOMO YA BIBLIA:** Matendo 16:29-34; Warumi 6:1-4

Jamaa ya Samweli ilikuwa na hamu kuu. Kila mmoja aliamka asubuhi na mapema wakati wa Jumapili. Hii ilikuwa siku ambayo ndugu mkubwa wa Samweli alikuwa anaenda kubatizwa.

Samweli hakuwa amewahi kusikia ibada ya ubatizo. Alikuwa na hamu ya kujua jinsi inavyoendeshwa. Aliuliza maswali mengi sana: "Je! watamfanyaje Yoshua? Je! watampeleka wapi? Je! "ubatizo" unamaanisha nini?"

Mamake Samweli alikuwa mwanamke mzuri Mkristo. Alimpenda Bwana kwa moyo wake wote. Alijua kwamba Samweli alitaka kujua yote yanayohusu ubatizo. Mama yake alifikiria kwamba huu ungekuwa wakati mzuri kwa Samweli kujionea mwenyewe maana ya ubatizo na pale ambapo ungefanyiwa. Hata hivyo, alimwambia kwamba "Ngojea na uone."

Mwishowe walikwenda hadi kule mtoni ambako Yoshua angebatiziwa. Walipofika huko walimkuta mchungaji akiwa majini akimngojea Yoshua na vijana wengine wawili ambao walitakiwa wabatizwe.

Alimwita Yoshua na kumwambia aingie majini. Yoshua alimwangalia ndugu yake Samweli, na akataba-samu. Aliingia majini kwa utaratibu na kumwendea mchungaji. Hatimaye



mchungaji yule alimnong'onezea Yoshua kile ambacho kingefanyika wakati wa kubatizwa.

Mchungaji huyo alikariri kifungu cha Biblia. Alimwekea mkono wake kichwani na akamwingiza majini. Mwili wote wa Yoshua ulifunikwa na maji.

Samweli aliendelea kufungua macho yake zaidi. Aliacha kupumua kwa mshangao alipomwona Yoshua akiingizwa majini. Alifikiri kwamba ndugu yake angezama. Lakini alianza kufurahi alipomwona ndugu yake akisimama akiwa majini na kuanza kutembea kuelekea ukingoni.

Baadaye waliporudi nyumbani, Samweli alimwuliza mamake kuhusu kubatizwa kwa Yoshua.

"Mama, Je! inamaana gani kubatizwa?" akauliza.

"Mtu hupatizwa baada ya kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wake," mamake akamwambia.

"Je! unakumbuka wiki chache zilizopita wakati Yoshua alipomwambia mchungaji kwamba anataka kuwa Mkristo?"

"Ndiyo," Samweli akamjibu.

"Sasa, ubatizo ni kitendo ambacho Mkristo mpya hufanya kwa kumtii Yesu," mamake akamwelezea. "Yesu alibatizwa ili kuwa mfano wetu. Wote wanaomwamini kama Mwokozi wao wanapaswa kufuata mfano huu."

"Leo nilipokuwa nikibatizwa, mchungaji alizungumzia juu ya kufia maisha ya kale na kufufuka kutoka

kwa wafu. Je! alikuwa akimaanisha nini?" Yoshua alimwuliza mamake aliyekuwa amekaa karibu naye.

"Mchungaji alikuwa akimaanisha kwamba mtu awapo Mkristo huwa hataki kufanya maovu aliyokuwa akifanya hapo zamani. Huiacha hali yake ya maisha ya zamani na yale aliyokuwa akifanya. Je! unakumbuka wakati mchungaji alipomwingiza Yoshua majini mpaka mwili wake wote ukafunikwa na maji?" mamake akamwuliza.

"Ndiyo, hata niliogopa kwamba Yoshua hatatoka tena majini," Samweli akasema. "Kwanza niliogopa kwamba anaenda kuzama."

Samweli alifikiria kwa dakika chache halafu akauliza, "Tuseme hata Yoshua naye alizikwa?"

"Ndiyo," mamake akamjibu. Halafu akaendelea, "Yoshua alipotoka majini, ilikuwa tu kama amefufuka kutoka kwa wafu. Ilikuwa kama amepata maisha mapya. Yesu alimpa maisha haya mapya, alipomsamehe Yoshua dhambi zake."

"Nako kutoka majini kwa Yoshua kulikuwa kama kufufuka kutoka kwa wafu, ama sivyo?"

"Mama! Je, Yoshua angebatizwa iwapo hajapata kuwa Mkristo?" Samweli akauliza.

"La," mamake akamjibu. "Ubatizo hauondoi dhambi. Mtu huokolewa kwanza kabla ya kubatizwa."

"Asante mama kwa kunieleza habari za ubatizo." Samweli akasema. "Nafikiri nitaongea na Yoshua jinsi

anavyojisikia baada ya kuwa Mkristo.”

Pengine unashangaa iwapo Wakristo wa kwanza walibatizwa. Tunajifunza kutoka katika kitabu cha Matendo kwamba walikuwa na ubatizo. Wiki iliyopita ulijifunza kwamba watu wapatao elfu tatu walibatizwa.

Sura ya 16 inatuelezea jinsi mlinzi wa gereza na jamaa yake walivyo-okolewa na hatimaye kubatizwa. Paulo na Sila walikuwa gerezani. Walikuwa wakiomba na kuimba nyimbo. Hatimaye kulitokea tetemeko la ardhi ambalo lilifungua milango ya gereza na kuilegeza minyororo ambayo wafungwa walikuwa wamefungiwa. Wakati mlinzi wa gereza alipoona kilichofanyika, alikuwa na uhakika kwamba wafungwa wote wametoroka. Alikuwa tayari kujua kwa sababu alijua kwamba angeadhibiwa vikali kwa kuwaacha watoroke. Paulo alimpazia yule mlinzi sauti kuu na kumwambia kwamba asijidhuru kwa sababu wafungwa wote walikuwa wangali wapo.

Mlinzi wa gereza alitaka kujua jinsi atakavyoweza kuokoka. Paulo na Sila walimwelezea mpango wa Mungu wa wokovu, yeye pamoja na nyumba yake yote. Wote walianini. Baadaye wote walioamini walibatizwa usiku huo huo. Soma vifungu vilivyoko katika somo la (Matendo 16:29-34).

Hata Yesu alibatizwa wakati wa mwanzo wa huduma yake. Yesu hakutenda dhambi. Hakutakiwa kutubu na kubatizwa. Lakini

alipobatizwa alitupa mfano wa kufuata. Alikuwa pia akijitambulisha kwa wanadamu waovu ambao alikuja kuwatumikia.

Warumi 6:1-4 inaeleza maana ya ubatizo. Soma vifungu hivi. Hebu mfikirie mtu ambaye anabatizwa. Mtu huyo anaingizwa ndani ya maji halafu anainuliwa tena. Hii ni picha ionyeshayo kile kilichofanyika maishani mwake. Wakati anaingizwapo ndani ya maji ni kama kuzikwa. Wakati anapoinuliwa kutoka majini ni kama kufufuka kutoka kwa wafu. Ubatizo ni ishara ya kuonyesha kufa na kufufuka. Mtu hufia aina moja ya maisha na kufufuka katika maisha mengine. Hufia maisha ya zamani ya dhambi na hufufuka katika maisha mapya ya neema.

#### KAZI YA KUFANYA

Weka alama (✓) kando ya jibu lililo sahihi.

Yoshua alibatizwa

\_\_\_\_\_akiwa nyumbani.

\_\_\_\_\_karibu na maji.

\_\_\_\_\_mtoni.

Chora mviringo kwenye jibu lililo sahihi.

Yoshua alibatizwa na

mchawi.

babu yake.

mchungaji wake.

shemasi.

Jaza nafasi zilizoachwa za vifungu hivi:

1. "Basi\_\_\_\_\_pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake..." (Warumi 6:4a).
2. "Hasha! Sisi tulioifia dhambi \_\_\_\_\_ tena katika dhambi?" (Warumi 6:2).
3. "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika\_\_\_\_\_yake?" (Warumi 6:3).

Andika majina ya watu wawili waliokuwa katika Matendo 16:25 ambao walikuwa gerezani.

\_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_

Jibu swali lifuatalo:

Je? Ni lazima mtu afanye nini kabla hajabatizwa? \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo" (Wagalatia 3:27).**

Mtu anapompokea Kristo kama Mwokozi wake huacha kabisa maisha yake ya zamani. Huanza maisha mapya. Ubatizo huonyesha picha ya kila kilichofanyika katika maisha ya Kristo. Kuingizwa kabisa katika maji huonyesha picha ya "kuzikwa" kwa maisha ya zamani. Anapoinuliwa kutoka majini, ni kama "kufufuka kutoka kwa wafu" kwa sababu ana maisha mapya.

Yesu alifia dhambi zetu. Halafu akafufuka kutoka kwa wafu. Mtu anapokuwa Mkristo hufia dhambi na kuanza maisha mapya. Wakati anapobatizwa huwa anamtii Yesu na kuonyesha wenzake kilichofanyika maishani mwake.



**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**  
**MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**  
**TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**  
**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

**SURA YA SITA**  
**CHAKULA CHA BWANA**

**MASOMO YA BIBLIA:** Mathayo 26:17-19, 26-28; I Wakorintho 11:23-29

Mji wa Yerusalemu ulikuwa umejaa watu. Kila mmoja alikuwa akijitayarisha kwa sherehe ya Pasaka. Wakati huu Wayahudi walikula mkate usiwekwa chachu na kutoa dhabihu ya mwana-kondoo. Wanafunzi walimwendea Yesu na kumwambia, "Bwana, leo ni siku ya muhimu sana katika historia ya taifa letu. Ni siku ambayo tunakumbuka jinsi Mungu alivyowakomboa babu zetu kutoka utumwani kule Misri. Huwa tunatayarisha chakula cha Pasaka ili kusherehekea siku hii. Ni lini unapotaka tule chakula hiki cha Pasaka?"

Yesu aliwaangalia huku akitabasamu na akawaambia, "Enendeni mjini na mtakutana na mwanamume ambaye amebeba mtungi wa maji. Mfuateni hadi katika nyumba


ataingia. Mwambieni mtu huyo kwamba mimi na wanafunzi wangu tutasherehekea Pasaka nyumbani kwake. Mtu huyo atawaonyesha chumba kikubwa. Tayarisheni Pasaka humo." Wanafunzi hao walifanya kile ambacho Yesu aliwaambia.



Usiku huo wakati walipokula pamoja Yesu aliuchukua mkate na akaubariki. Aliumega katika sehemu ndogo ndogo na akawapatia wanafunzi wake. Akawaambia, "Twaeni mle." "...huu ndio mwili wangu uliotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu." (Luka 22:19)

Baadaye Yesu alichukua kikombe cha divai na akakibariki.

"Nyweni nyote katika hiki;" akawaambia, "kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi." (Mathayo 26:27-28)



Mkate ni mfano wa mwili wa Yesu ambao ulivunjwa kwa ajili yetu. Nayo divai ni mfano wa damu ya Yesu ambayo ilimwagika kwa ajili yetu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kukumbuka kifo chake kwa kuwa na Chakula cha Bwana. "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu," (Luka 22:19) akawaambia. Soma katika Mathayo 26:17-19, 26-28 ili uone kile ambacho Yesu alisema.

Je! siku hizi Wakristo wanakumbukaje kifo cha Yesu? Hukumbuka kifo cha Yesu kwa kuwa

na Chakula cha Bwana. Hula Chakula cha Bwana ili kukumbuka jinsi Yesu alivyojitua mwili na damu yake ili kutusamehe dhambi zetu.

Wakristo wanashiriki katika Chakula cha Bwana hula mkate ili kujikumbusha mwili wa Yesu, na hunywa divai ili kujikumbusha damu ya Yesu. Wakati huu, Wakristo humfikiria Yesu na jinsi alivyotoa maisha yake ili kutusamehe dhambi zetu. Yule ambaye si Mkristo hapaswi kushiriki katika Chakula cha Bwana, kwa sababu hakitakuwa na maana kwake.

Chakula cha Bwana huwa wakati wa kuabudu. Mkristo anapokumbuka upendo mkuu wa Mungu, hutaka kutoa maisha yake ili amtumikie tu Mungu. Chakula cha Bwana si kama chakula cha kawaida. Ni wakati wa kutulia, na kuomba na kukumbuka upendo wa Mungu.

Kanisa la Wakorintho walikuwa na sherehe ya upendo ambayo ilitangulia sherehe ya Pasaka. (Soma 1 Wakorintho 11:20-22) Watu walipenda sana wakati maalum walipokula vyakula pamoja. Hata hivyo, sherehe hii ya upendo ilikuwa na maana tofauti katika kanisa la Korintho. Chakula hiki kilitakiwa kiwe cha kukumbuka jambo la kidini, lakini kilisherehekewa kwa njia mbaya sana. Badala ya kushiriki pamoja, wale waliokuwa matajiri walikuja mapema kanisani na kuleta chakula chao. Walianza kula kwa haraka kabla maskini hawajafika. Kwa kweli, hawakupaswa kula Chakula cha Bwana ambacho kilifuatia sherehe ya upendo.

Chakula cha Bwana si karamu. Hakimfanyi mtu kuwa mwema. Chakula cha Bwana ni cha kukumbuka yale ambayo Yesu alitufanyia alipokufa msalabani.

Watu wengine hudhani kwamba hawafai kula Chakula cha Bwana. Kila Mkristo ana dhambi maishani mwake. Lakini anapaswa kuwa akimwomba Mungu amsamahe dhambi zake. Mungu tu ndiye awezaye kutufanya tufae kukaa mezani pake. Kila Mkristo anapaswa kuja kwa moyo wa kutubu dhambi zake na kumwomba Mungu amfanye afae badala ya kukaa mbali.

Wakati mwingine vijana Wakristo huona kama kwamba hawapaswi kushiriki katika Chakula cha Bwana. Wao huondoka kanisani kabla mchungaji hajaanza ibada hii. Ikiwa umempokea Kristo kama Mwokozi wako, na umebatizwa na kuwa mshiriki wa kanisa, una wajibu wa kushiriki katika Chakula cha Bwana.

Wiki iliyopita ulijifunza kuhusu ubatizo. Ubatizo na Chakula cha Bwana vinajulikana kama agizo la kanisa. Agizo ni sharti au amri ya Yesu ambayo ingali inafuatwa hata sasa.

Nawe je? Je! unashiriki katika Chakula cha Bwana katika kanisa lako? Unapaswa kufuata mfano wa Yesu ili ushiriki kwa ukamilifu.

#### KAZI YA KUFANYA

Chora msitari kutoka kwa usemi wa kwanza uhusuo chakula cha Bwana hadi kwa usemi wa pili ili ukamilishe sentensi hii.

sherehe.

wakati wa kuzu-ngumza na marafiki.

wakati wa kuku-mbuka yale ambayo Yesu ametufanyia alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Chakula cha Bwana ni

---

mwili wa Yesu.

Mkate ni mfano wa

kwamba kila mmoja anapaswa kula mkate wakati wa sherehe.

kuwa na njaa.

---

Divai ni mfano wa

damu ambayo Yesu alimwaga kwa ajili ya dhambi zetu.

maji ambayo hayawezi kutuokoa.

Jibu maswali yafuatayo:

1. Je! makanisa mengi ya kibatisti hutilia maanani maagizo mangapi? \_\_\_\_\_
2. Je! maagizo haya ni yapi? \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_
3. Je! Yesu alishiriki kwanza Chakula cha Bwana na akina nani? \_\_\_\_\_
4. Je! ni nani ambaye tunapaswa kukumbuka wakati tunapokula Chakula cha Bwana? \_\_\_\_\_

5. Je! unadhani ni nini ambacho mtu anapaswa kukumbuka kuhusu Yesu wakati anapokula Chakula cha Bwana. \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_

**Kamilisha kifungu hiki cha Biblia:**

“Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza \_\_\_\_\_ ya Bwana hata ajapo.” (1 Wakorintho 11:26)

Chora mviringo kwa vitu vile ambavyo vinahitajika kwa ajili ya Chakula cha Bwana.

Mkate divai mahindi tofaa  
Wakristo

#### **KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

“Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo” (1 Wakorintho 11:26).

Yesu aliwataka Wakristo washiriki katika Chakula cha Bwana mara kwa mara. Lakini hakuna wakati maalumu ambapo wanapaswa kula Chakula cha Bwana. Mekanisa mengi hushiriki Chakula cha Bwana baada ya miezi mitatu. Lakini kila wakati walapo Chakula hiki, wanapaswa kumfikiria Yesu na mwili wake na damu ambayo alitoa kwa ajili yetu.



**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**  
**MWAKA WA TATU KITABU CHA TATU**  
**TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**  
**J3 - 3Ps**

Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

**SURA YA SABA**  
**VIONGOZI WA KANISA**

**MASOMO YA BIBLIA: I**  
Wakorintho 12:4-11; Matendo 6:1-6

Leo tutawahoji wazee kadhaa wa kanisa. Tunataka tuwaulize watwambie kazi wafanyazo kanisani. Hebu tuongee na mzee wa kwanza.

**Msimulizi:** "Hujambo bwana! Karibu katika kipindi chetu cha redio. Je! wewe ni nani?"



**Mchungaji:** "Sijambo. Mimi ni mchungaji. Huwaongoza watu wa kanisa langu. Njia moja nifanyayo hivi ni kwa kuhubiri kutoka kwa Neno la Mungu kila Jumapili wakati wa Ibada. Mungu hunisaidia kujua kile ambacho napaswa kuliambia kanisa wakati ninapohubiri.

"Mimi huwatembelea pia wagonjwa, wenye mahitaji, waliofiwa, maskini na matajiri walioko katika kijiji chetu. Hasa wagonjwa wanapaswa kujua kwamba Mungu anawapenda na kuwatunza. Wanapaswa pia kujua kwamba watu wa kanisa wanawapenda na huwajali.

"Wakati mtu anapokufa katika kijiji chetu, mimi huenda na kuifariji jamaa hiyo. Au wakati nyumba fulani inapotekekea kwa moto, mimi huenda na kuwafariji waliopatwa na shida hiyo. Watu wengine wanapaswa kujua kwamba

washiriki wa kanisa wanawajali wanapopatwa na shida. Mimi huwashauri watu ambao wanashida nyumbani kwao au kazini kwao. Hujaribu ili waone kile Biblia isemacho kuhusu shida zao.

“Mimi kama mchungaji, nina wajibu wa kuwasaidia washiriki wakue kiroho. Kila Mkristo anapaswa kusoma. Huwasaidia washiriki wa kanisa kuweza kutambua nafasi ya kuwashuhudia wale ambao si Wakristo. Huwafundisha jinsi ya kuwa mawakili wema wa wakati wao, pesa na uwezo walionao.”

**Msimulizi:** “Asante sana Mchungaji. Sasa ni wakati wa kuzungumza na mzee mwingine. Hujambo Bwana! Je! wewe ni nani?”

**Shemasi:** (Anakohoa kwanza) “Mimi ni shemasi. Nami humsaidia mchungaji. Huwatembelea wagonjwa, wale waliofiwa, na wale wanaohitaji mtu wa kusema nao. Huwakaribisha watu wa kijiji chetu kuja kanisani. Kuna wakati huwa naenda na mchungaji na wakati mwingine mimi huenda peke yangu kuwashuhudia wale wasio Wakristo. Humsaidia mchungaji wakati kanisa letu linapokuwa na Chakula cha Bwana. Mimi huwapatia washiriki mkate na divai. Husaidia pia katika mikutano ya kanisa na mambo mengine yanayohusu kanisa. Hulisaidia kanisa kuwa kile ambacho linapaswa liwe. Wakati mwengine washiriki huhitaji kutiishwa, kwa hivyo hufanya kazi na mchungaji na washiriki wengine

ili kuwakumbusha watu hawa jinsi Mkristo anavyopaswa kuishi.”

**Msimulizi:** “Asante sana shemasi, Asante kwa kutuambia kile ufanyacho kanisani. Namwona mwanamke mmoja akija. Hujambo! Je! wewe hufanya nini kanisani?”

**Mwalimu wa Shule ya Jumapili:** “Sijambo. Mimi ni mwalimu wa Shule ya Jumapili. Huwa nawafundisha washiriki wa darasa langu kila Jumapili, kuhusu ujumbe wa Mungu. Huwasaidia wanafunzi wangu kuelewa yale ambayo Biblia inatuambia. Kufundisha Shule ya Jumapili ni kazi muhimu sana. Ni lazima kila wiki nitumie muda mwingi kusoma somo la Biblia ili niweze kufundisha darasa langu vyema. Ni lazima nijue mahitaji ya wanafunzi wangu na niwaombee. Ni lazima pia nifike kanisani asubuhi na mapema ili niweze kuwa-karibisha wanafunzi wangu.

“Huwatembelea washiriki wa darasa langu ambao wamekosa kufika na watu wengine ambao wangependa kujiunga na darasa hilo. Kutembelea ni kwa muhimu sana kwa kiongozi ye yote wa kanisa. Ninapotembelea huweza kukutana na jamaa za wale ambao ninawafundisha. Nami hupata nafasi ya kuweza kuwashuhudia.

“Wakati mwingine ni vigumu kuwa mwalimu wa Shule ya Jumapili. Na ni muhimu kwetu kama waalimu wa Shule ya Jumapili kuishi kulingana na yale tunayofundisha. Ni lazima tuwe wema na wenye upendo na tumtii

Mungu, jinsi tunavyo wafundisha wanafunzi wetu kufanya.”

**Msimulizi:** “Asante kwa kuzungumza nasi. Namwona mtu mwingine akija. Hujambo Bwana! Je! wewe ni nani?”

**Kiongozi wa Nyimbo:** “Mimi ni kiongozi wa nyimbo. Mimi huwaongoza watu kuweza kuimba wakati wa Ibada. Uimbaji ni njia muhimu ya kumtukiza Mungu. Ni sehemu muhimu ya Ibada.”

**Msimulizi:** “Asante kwa kutuambia kazi ufanyayo kanisani. Si rahisi kuongoza nyimbo wakati wa ibada. Tutakuombea katika kazi hii. Namwona pia mtu mwingine akija. Hujambo Bwana! Je wewe ni nani?”

**Bawabu:** “Sijambo. Mimi ni bawabu. Kazi yangu si ngumu sana, lakini inahitaji kusimama mara kwa mara. Mimi huwapatia washiriki vitabu vya nyimbo. Baadaye, huenda kusimama mlangoni ili niwa-karibishe watu wanaofika na niwaonyeshe mahali pa kukaa. Napenda kazi yangu kwa sababu hunipa nafasi ya kuweza kukutana na watu mbali mbali.”

**Msimulizi:** “Asante sana kwa kuzungumza nasi leo. Huyu ni msimulizi wenu akiwaaga na kusema kwaherini hadi tutakapokutana wakati mwingine.”

Watu uliokutana nao leo wanaitwa viongozi wa kanisa. Lakini kuna kazi ambayo kila mshiriki wa kanisa anapaswa kufanya. Wana kwaya wanahitaji kuongoza ibada kwa nyimbo. Watu wengine wanahitajika

kulifanya kanisa kuwa safi na kukata nyasi. Mungu amempa kila Mkristo karama moja ambayo inaweza kutumiwa ili kumhudumia na kulijenga kanisa.

Soma Maandiko ya somo letu la leo kutoka katika I Wakorintho 12:4-11. Vifungu hivi vinatuambia kwamba Mungu hutupa karama za Roho ambazo tunapaswa kufanyia kazi yake. Mtu hapaswi kujivuna kwa sababu amechaguliwa kuwa kiongozi katika kanisa. Mungu humpa karama ya kuongoza ili awatumikie wengine.

Vifungu vya Matendo 6:1-6 vinatwambia kuhusu wasaidizi wa kwanza waliochaguliwa na kanisa la Agano Jipya. Kanisa lilikuwa na shida. Washiriki waliozungumza Kiyunani walilalamika kwamba wajane wa Kiyunani hawakuwa wakitendewa mema. Mitume waliwaita waamini wote pamoja. Waliyafikiria hasa mahitaji ya wajane hawa. Lakini wao walisema kwamba Mungu alikuwa amewaita hasa kuomba na kuhubiri.

Mtu mmoja alidokeza kwamba washiriki hao wachague watu saba kati yao ambao wangeshughulikia jambo hili. Walipaswa wawe wale ambao wamejawa na Roho Mtakatifu.



Watu hawa saba huitwa mashemasi wa kwanza. Biblia haitumii neno hili inapozungumzia juu yao, lakini mashemasi wa sasa hufuata mfano wa wale wa kwanza saba wanapohudumia kanisa.

### KAZI YA KUFANYA

Chora mstari kutoka kwa jina la kiongozi wa kanisa hadi kwa usemi ambao unaeleza kazi ambayo yeye hufanya.

Mchungaji      hufundisha Biblia kila Jumapili.

Shemasi        huongoza nyimbo wakati wa ibada.

Mwalimu wa Shule ya Jumapili      huhubiri na kutembelea.

Kiongozi wa Nyimbo      humsaidia mchungaji katika kutembelea na kutayarisha Chakula cha Bwana.

Kamilisha kifungu kifuatacho cha Biblia:

“Basi pana tofauti za \_\_\_\_\_, bali Roho ni yeye yule.” (1 Wakorintho 12:4)

Weka alama ya (✓) kando ya sentensi za kweli.

\_\_\_\_Ni lazima viongozi wamwombe Mungu na wamwulize msaada.

\_\_\_\_Ni lazima viongozi wawe na umri upatao miaka hamsini.

\_\_\_\_Viongozi hawapaswi kwenda kanisani mara kwa mara.

\_\_\_\_Ni lazima viongozi wawe na elimu.

\_\_\_\_Ni lazima viongozi watumike kwa sababu wanampenda Mungu, bali si kwa sababu ya majivuno.

Pangua herufi zifuatazo ili upate maneno yanayoeleza yule anayetoa karama na vipawa vyote. (1 Wakorintho 12:11)

HORO      TAMKAFUTI

---

### KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule, azitendaye kazi zote katika wote” (1 Wakorintho 12:6).

Viongozi wa kanisa wana karama tofauti. Wao huchaguliwa kufanya kazi tofauti kanisani. Mungu anawahitaji wote wamfanyie kazi. Anawataka viongozi wamtegemee. Anawataka wawe wapole, na wasijivune. Aliwapa viongozi hawa aina mbali mbali ya karama na vipawa ili waweze kumtumikia na kulijenga kanisa lake.



# **VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

## **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

## **SURA YA NANE**

### **MSHUHUDIE KRISTO -- NYUMBANI**

**MASOMO YA BIBLIA: Marko 5:1-20**

Yesu na wanafunzi wake walivuka Bahari ya Galilaya. Waliifikia nchi ya Gerasi ambako walianza kufanya kazi ya Mungu.

Waliposhuka kutoka mashuani, walikutana na mtu aliyekuwa na pepo wachafu. Hapakuwa na yeye ambaye alienda karibu naye. Wanafunzi walimwogopa, lakini Yesu haku-mwogopa. Mfu huyu aliishi makaburini, na alikuwa na nguvu nyingi. Hakuweza kufungwa kwa minyororo aliikatakata kutokana na nguvu zake. Hapakuwa na ye yote ambaye angeweza kumkataza kupiga kelele, wala kujikatakaka kwa mawe.

Yule mtu mwenye pepo wachafu alimwona Yesu na akamkimbilia ili amsujudie. Yesu aliwaamuru wale pepo wachafu wamtoke mtu yule. Halafu Yesu akauliza, "Jina lako nani?"

"Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi," akamjibu. Yesu aliwafanya pepo wale wachafu waingie nguruwe waliokuwa karibu. Nguruwe hao walitelemka kwa kasi sana na wakatumbukia baharini. Nguruwe wapatao elfu mbili walikufa baharini, lakini yule mtu mwenye pepo wachafu aliweza kuponywa.



Mchungaji wa nguruwe wale aliogopa sana. Alizunguka mjini na hata nchini kote akiwaambia watu yote aliyokuwa ameona.

Watu walienda hadi mahali ambapo Yesu alikuwa. Waliwaona wanafunzi wake na yule mtu ambaye alikuwa

ameponywa. Alikuwa amevaa nguo na mwenye akili timamu. Alikuwa ameponywa na Yesu.

Watu walioishi katika eneo lile waliogopa sana na wakamtaka Yesu aondoke. Walikuwa na hasira ya kuwapoteza mifugo wao hata ingawa mmoja wao alikuwa ameponywa.

Watu waliuliza maswali juu ya mwujiza huu: Je! huyu ndiye mtu aliyekuwa na pepo wachafu ambaye alikuwa akiishi makabuni?" "Aliponywaje?" Walikuwa wanamfahamu mtu huyu mwenye pepo wachafu kabla hajakutana na Yesu. Sasa alikuwa amebadilika sana.



Wakati Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wanajitayarisha kuingia mashuani, mtu huyu aliyeponywa alimwuliza Yesu iwapo angeenda pamoja nao. Alitaka amsaidie Yesu.

Yesu alikataa. Akamwambia, "Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu." (Marko 5:19)

Yesu angemwalika mtu yule kwenda naye kwa sababu alihitaji wasaidizi. Naye angemsaidia Yesu na wanafunzi

wake kufundisha na kuwashuhudia watu wa sehemu zingine. Lakini Yesu alimwambia mtu yule kurudi kwao na kuiambia jamaa yake pamoja na marafiki yale ambayo Mungu amemfanyia.

Yesu alijua kwamba mtu yule angeshuhudia vizuri kwa kuwa pale alipokuwa. Jamaa na marafiki zake walimjua vizuri sana. Walijua habari za ugonjwa wake na wangeona jinsi Yesu alivyokuwa amemponya. Hakuna ye yote ambaye angeelezea vizuri kile kilichofanyika kuliko yeye mwenyewe.

Yesu alikuwa amempatia maisha mapya. Kabla ya kuponywa, hakuwa na jamaa wala marafiki ambao wangemsaidia. Pepo wachafu walimharibu akili yake hata hakuweza kufikiria vizuri. Hakuvaa nguo wala kujitunza vizuri. Alikuwa na shida nyingi sana, naye Yesu alikuwa amemponya na kumpa maisha mapya.


Yule mtu aliyeponywa alienda na kuwambia wengine habari za Yesu. Je! unaweza kufikiria mshangao ambao watu waliomsikia akisema walikuwa nao walipomwona akiwa amebadili matendo yake? Haikosi wali-mwangalia na kuzungumzana kati yao kuhusu mabadiliko yake.

Huenda watu wa Gerasi walisema kwamba, "Ningependa kumjua Yesu, ambaye alimponya mtu mwenye pepo wachafu. Najua anaweza kunisaidia pia."

Yesu anatutegemea sisi tumshuhudie jinsi alivyomtegemea mtu yule aliyekuwa ameponywa. Anatutaka tuwaambie walioko

nyumbani, shuleni, sokoni, na majirani yale ambayo ametufanyia maishani mwetu.

Yesu alijua kwamba kila Mkristo hangeweza kwenda sehemu nyingine ya nchi yake, au katika nchi ya kigeni ili kuwaambia wengine habari zake. Lakini kila Mkristo anaweza kuwaambia watu walioko karibu naye habari za Yesu.



Wakristo hushuhudia pia kutokana na matendo yao, sio tu kwa yale wasemayo. Kwa mfano, wale ambao wanadai kuwa Wakristo, hali wanaiba na kuwatukana wenzao huwa si mashahidi wema wa Yesu.

Wafuasi wa Yesu waliitwa kwanza “Wakristo” kwa sababu walikuwa “kama Kristo.” Walikuwa watu waliosema na kutenda kama Yesu.

Je! wewe ni shahidi wa Yesu pale ulipo? Msikilize Yesu anapokuambia, “Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu.” (Marko 5:19) Anza leo kuwaambia wengine habari za Yesu.

## KAZI YA KUFANYA

Soma Marko 5:9. Andika vizuri herufi zifuatazo ili upate jina la mtu yule mwenye pepo wachafu.

### GIELINO \_\_\_\_\_

Jaza nafasi iliyoachwa na jibu lililo sahihi.

1. “Na alipokwisha kushuka chomboni, mara alikutana na mtu, ambaye ametoka makaburini, mwenye \_\_\_\_\_ mchafu.” (Marko 5:2)
2. Mara kwa mara mtu huyu alikuwa akifungwa kwa \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_ (Marko 5:4)
3. Je! mtu yule mwenye pepo wachafu alijikatakata akitumia nini? \_\_\_\_\_ (Marko 5:5)
4. Je! Mtu yule alifanyaje alipomwona Yesu? (Marko 5:6) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
5. Je! pepo wale wachafu walienda wapi baada ya Yesu kuwatolea kutoka katika mtu yule? (Marko 5:13) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
6. Je! ni nguruwe wangapi waliokufa baharini? (Marko 5:13) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

Weka alama (✓) kando ya sentensi ya kweli na upige mstari katika sentensi ambayo si kweli.

\_\_\_\_ Mkristo anaweza kushuhudia tu katika nchi ya mbali.

\_\_\_\_ Yesu alimwambia mtu yule mwenye pepo wachafu kurudi nyumbani kwao na awaambie rafiki zake yale ambayo Yesu alikuwa amemfanyia.

\_\_\_\_ Mkristo hapaswi kuiambia jamaa na marafiki zake za habari za Kristo.

Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kutumia maneno yako mwenyewe:

Samweli alipata kuwa Mkristo wakati wa mkutano wa ufufuo uliofanywa katika kijiji chake. Baadhi ya marafiki zake walianza kumchokoza aliporudi shuleni. Walimchekelea huku wakimwambia, "Tulisikia kwamba ulimpokea Kristo wiki iliyopita. Ukristo haufai vijana hodari kama sisi. Unafaa tu wanawake na wasichana."

Samweli akawaambia, " \_\_\_\_\_

---

---

---

---

---

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"...Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kweni, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu" (Marko 5:19).**

Yesu alijua kwamba mtu yule aliyeponywa alikuwa na ushuhuda wa kusema ambao mtu mwingine ye yote hangeweza kuutoa. Alimwambia awaambie ushuhuda huo watu wa jamaa yake na marafiki.

Andika majina ya marafiki wanne ambao unajua wanataka kumfahamu Yesu. Anza kuwaomba wiki hii. Uwe tayari kushiriki ushuhuda wako nao jinsi Bwana atakavyo kuongoza.

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_



# **VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

## **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

## **SURA YA TISA**

### **MSHUHUDIE KRISTO -- KWA MAJIRANI**

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo**  
**10:24-39**

Siku moja Monika alikuwa akimsaidia mama yake kusaga mahindi. "Mama," akasema. "Tulipokuwa kanisani jana mchungaji

alizungumzia kuwasaidia wengine. Alisema kwamba tunapaswa kuwatembelea wengine, kuwashuhudia, kuwasaidia na kuwaonyesha kwamba Mungu anawapenda. Je! mchungaji alimaanisha nini kwa kusema kwamba tuwashuhudie wengine kwa kuwasaidia?"

Mama yake akamwambia, "Monika, alikuwa akimaanisha kwamba tuwasaidie wenzetu ili wajue kwamba tunawapenda na pia, Mungu anawapenda. Kwa mfano, tunaweza kumpelekea chakula jirani yetu aliye mgonjwa. Yeye ni mgeni katika nchi yetu. Jamaa yake iko mbali katika nchi yao, naye huongea lugha tofauti na yetu na hana mtu kwake ambaye anaweza kumtunza. Tunaweza kusaidia halafu tumwambie habari za Yesu."

"Lakini, mama, mimi nitafanya nini?" Monika akauliza. "Sitajua kitu cha kufanya. Hata nitaona haya kwenda huko peke yangu.. Je! nitamwambia nini?"



“Unaweza kuwa msaada mkubwa sana,” mama yake akamjibu. “Hupaswi kuwa mkubwa ili umtumikie Mungu. Mungu ana kitu ambacho unaweza kufanya. Hebu tumtembelee leo jioni na tumpelekee chakula. Utanisaidia kukipika, na ninauhakika kwamba Bwana atatuonyesha jinsi ya kutumia jambo hili kama ushuhuda.”

Mamake akaendelea, “Kuna wengine ambao unaweza kuwasaidia. Kwa mfano, mkewe Dube aishiye karibu na mto ni mzee sana wa kutoweza kwenda kutafuta kuni wala kuteka maji. Je! Unafikiri unaweza kumsaidia? Unafikiriaje kuhusu yule msichana mgeni uliyenieleza habari zake, ambaye alikuwa darasani mwenu. Bila shaka anahitaji rafiki, nawe unaweza kuwa rafiki huyo.”

“Mama, sikuwa nimewafikiria kamwe,” Monika akasema. “Ni watu ambao naweza kuwasaidia, huku nikiwaambia kwamba Yesu anawapenda. Mama, naweza kwenda nyumbani kwa mkewe Dube jumamosi asubuhi ili nimsaidie?” Mama yake akamjibu. “Bila shaka, unaweza kwenda.”

“Nilifanya urafiki na Sara, yule msichana mgeni,” Monika akasema, “Lakini sasa nataka kutafuta njia ambazo naweza kumsaidia ili asijisikie kuwa pweke.”

“Kuna watu wengi ambao wewe na wenzako wa kanisa mnaweza kuwasaidia.” Mama yake akamkumbusha. “Baadhi ya washiriki wetu wa Shule ya Jumapili huwa wanamsomea Biblia yule mzee ambaye



hukaa katika kiti cha mbele cha kanisa kila Jumapili asubuhi. Yeye hawezi kusoma wala kuandika. Hawezi kuona vizuri kwa sababu ya umri wake. Hata hivyo, anampenda Mungu na hupenda kusikiliza anaposomewa Neno la Mungu.”

“Mama,” Monika akauliza, “Je! naweza kumshuhudia Kristo kwa kuwaambia tu? Je! kwa nini natakiwa kuwasaidia?”

“Unaweza,” Mamake akamwambia, “Lakini ushuhuda wako utafaa sana iwapo utawaambia na kuwaonyesha kwamba Mungu anawapenda. Kumbuka hadithi ya Yesu iliyoko katika Biblia. Aliwaambia watu habari za Mungu na akawasaidia pia. Sisi huwaonyesha wenzetu kuwa tu Wakristo kutokana na yale tusemayo na kutenda.

Mama yake akaendelea kusema, “Njia moja nzuri ya kushuhudia ni kwa kuwapenda wengine. Yesu alifundisha kwamba hivi ndivyo ulimwengu uwezavyo kujua kwamba tu wanafunzi wake. Yesu alitupenda na alionyesha upendo wake kwa yale aliyofanya. Vivyo hivyo, nasi tunapaswa kuonyesha kwa Mungu, kwa yale tufanyayo.”

“Nawapenda watu kadhaa, lakini sio wote,” Monika akasema. “Kuna mvulana mmoja darasani mwetu hupenda sana kunitega, au kuangusha vitabu vyangu. Hata ni vigumu kumpenda.”

“Kuna watu kama hao,” mamake akamwambia. “Si rahisi kumpenda kila mmoja. Lakini unaweza kumwomba Mungu akusaidie ili umpende hata ingawa huwa hakutendei mema. Mungu atakwonyesha upendo wa Kristo kwa yale ufanyayo.”

Walimaliza kusaga mahindi na wakawa tayari kuanza kupika. Monika na mamake waliwasha moto ili wapike chakula ambacho wangempelekea jirani yao aliye mgonjwa.



## KAZI YA KUFANYA

Chora mstari kutoka mwanzo wa sentensi hadi kwenye ile sehemu iliyo ya kweli.

Shahidi ni mtu ambaye hapendi ugomvi.

mtu ambaye anawaambia habari za upendo wa Mungu kwa matendo na yale asemayo.

yule anayefanya kazi ya upishi.

Weka alama (✓) kando ya sentensi iliyo sahihi.

—Monika hakisikiliza yale ambayo aliambiwa na mchungaji wake.

—Monika alitaka kujua jinsi alivyotakiwa kuwashuhudia wenzake na kuwasaidia.

—Monika alitaka tu kuongea na mama yake ili asifanye kazi ya kusaga mahindi.

Chora mviringo kwenye mambo yale ambayo unaweza kufanya ili uwasaidie wale wasio Wakristo kujua kwamba unawapenda na pia Mungu anawapenda.

1. Nimsaidie mama mzee kubeba kuni.
2. Niwachokoze watoto wa jirani na kuwafanya walie.
3. Nimsomee kipofu Biblia.
4. Nifiche kifaa cha mtoto cha kuchezea.

5. Nimpelekee mama mgonjwa chakula.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo 1:8).**

Je! Yesu anatupa nani ambaye atatusaidie kumshuhudia?

R\_\_\_\_\_ M\_\_\_\_\_

Je! Yesu aliwaambia wanafunzi wake wamshuhudie wapi?

Katika Y\_\_\_\_\_, na katika U\_\_\_\_\_ wote, na S\_\_\_\_\_ na hata mwisho wa nchi.

Yesu alikuwa Yerusalemu pamoja na wanafunzi wake alipowaamuru hivi. Kwa hivyo, aliwataka waanze kushuhudia pale walipo. Andika jina la kijiji au mji wako katika nafasi ifuatayo. Hii ndiyo Yerusalemu yako.

Uyahudi ilikuwa ni pamoja na eneo lote ambalo lilitumia Yerusalemu kama mji mkuu. Andika baadhi ya majina au miji ambayo iko katika eneo lako au mkoa wako.

---

---

---

---

---

---

Yesu anawataka wafuasi wake kushuhudia pia katika sehemu hizi.

Samaria lilikuwa eneo ambalo lilikuwa mbali na lenye desturi tofauti na za Uyahudi. Hasa watu wa Mataifa ndio walioishi Samaria, nao Wayahudi hawakuwa marafiki na Wasamaria. Andika majina ya nchi ambazo ni jirani na nchi yako.

---

---

---

---

---

---

Watu wa huko wanaweza kuwa wanaongea lugha tofauti. Pengine serikali ya nchi yako haiwezi kuwa na urafiki na serikali ya nchi jirani. Lakini Mungu yungali anawataka wafuasi wake kuwa mashahidi wa nchi hizo pia.

Mwishowe Yesu alisema twende hadi mwisho wa nchi. Kila mtu amehusishwa katika amri hii. Anawataka watu wote wajue upendo wa Mungu na wokovu ambao anawapatia kupitia kwa kifo chake pale msalabani.



## **VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA MWAKA WA TATU KITABU CHA TATU TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

### **SURA YA KUMI MSHUHUDIE KRISTO -- ULIMWENGUNI**

**MASOMO YA BIBLIA:** Mathayo  
28:18-20

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kabla ya kwenda mbinguni kuwa pamoja na Mungu kwamba, "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi



sikuzote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:19-20).

Tunaita maneno haya "Agizo Kuu". Ilikuwa amri kuu ya Yesu kwa wanafunzi wake na kwetu sisi. Anatutarajia kwenda ulimwenguni kwote na kuwa mashahidi wake.

Jumapili moja, Patrick alimsikia mchungaji wake akihubiri juu ya Agizo kuu la Yesu. Baada ya ibada alienda kuzungumza na mchungaji huyo. Akamwambia, "Mchungaji, najua kwamba Yesu alitwambia twende ulimwenguni na tuwe mashahidi wake, lakini, nawezaje kufanya hivyo?"

Mchungaji aliweka mkono wake juu ya bega la Patrick alipoendelea kusema, "Mimi ningali kijana. Hata siwezi kuacha shule na jamaa yangu ili kwenda katika sehemu za mbali na kuwaambia watu habari za Yesu."

Mchungaji huyo alitabasamu na akamwambia, "Mungu hakutarajii

kuondoka nyumbani kabla hujawa mkubwa. Jambo muhimu ambalo unaweza kufanya sasa ni kumaliza masomo yako. Lakini Mungu anakutaka umtumikie pale ulipo.”

“Ningependa sana kuwaambia wengine habari za Yesu.” Patrick akaongeza. “Ameniokoa na ninataka wengine wajue mabadiliko aliyofanya maishani mwangu.”

“Patrick, hebu niabie,” mchungaji akauliza. “Je! kuna wanafunzi katika shule yako ambao si Wakristo?”

“Je! unamaanisha nini?” Patrick akauliza.

“Sasa ni hivi,” mchungaji akaeleza. “Kristo anaweza kukutaka uwa-shuhudie baadhi ya wanafunzi wenzako ambao hawamfahamu.”

“Sijawahi kuwafikiria kamwe.” Patrick akasema pole pole. “Wanafunzi wa shule yetu huwa wanasikia habari za Yesu. Nilidhani kwamba Yesu alitutaka tuwaendee watu ambao hawajawahi kumsikia kamwe.”

Mchungaji akamwambia, “Nina-amini kwamba Yesu alitutaka tufanye yote mawili. Anataka watu wazima wengine waache jamaa na kazi zao na kuwaendea watu wa kabila au taifa lingine na kuwafundisha habari zake. Lakini anatutaka baadhi yetu tumshuhudie pale tuishipo.”

“Je! mchungaji sasa nitafanya nini?” Patrick akamwuliza.


“Pengine Mungu anakutaka uwe mchungaji, daktari, mmisheni au mwalimu,” mchungaji akamwambia. “Jambo upaswalo kufanya sasa ni kujitayarisha kwa kusoma kwa bidii.

Unapaswa uwe tayari kwa cho chote kile ambacho Mungu atakutaka ufanye.”

“Mimi ni mwanafunzi mzuri,” Patrick akaongeza. “Lakini najua kwamba ninaweza kuwa bora zaidi.”

“Unapaswa pia kuwa mwaminifu kwa kuwashuhudia wale unao-wafahamu, ambao hawajaokoka,” Mchungaji akasema. “Yesu hakutaki ungojee hadi utakapomaliza masomo yako ndipo uanze kushuhudia. Anataka kukutumia sasa hivi.”

Mchungaji aliendelea kueleza kwa kuchora mfano mmoja kwenye karatasi.



“Patrick, kuna njia nyingi ambazo unaweza kumshuhudia Kristo kwazo.” Njia moja ni kwa kumwambia mtu mwingine habari za Yesu wewe mwenyewe. Njia nyingine ni kwa kuwaomba wapotevu ili wapate kusikia injili. Nayo nyingine ni kwa kutoa katika kanisa lako ili kuwasaidia wamisheni ambao tunawatumia kupitia kwa jumuiya yetu.”

“Je! mchungaji unamaanisha nini unaposema jumuiya?” Patrick akauliza.

“Pengine ningekuchorea tena picha nyingine ya kukusaidia kuelewa jinsi tuwezavyo kuwatuma wamisheni,” mchungaji akamwambia. “Hebu nikuulize swali kabla sijaendelea. Je!

unafikiri kanisa letu lina pesa za kutosha za kumsaidia mmisheni?"

"La," Patrick akajibu. "Baba yangu huniambia kwamba huwa tunapata shida ya kulipa mshahara yako na kushughulika gharama za kanisa."

"Hiyo ni kweli," mchungaji akajibu. "Lakini kuna njia ambayo tunaweza kutumia. Tunaweza kuweka pesa zetu pamoja na zitoshe iwapo tutashiriki-ana na makanisa mengine kama hili letu."

"Hebu utazame mchoro huu ambao unaeleza kile ninachosema," mchungaji akaanza kuchora.

"Kuna makanisa yapatao elfu moja katika nchi yetu. Baadhi ya makanisa haya ni makubwa na mengine ni madogo. Kunayo yale ambayo yamewaajiri wachungaji na mengine yana wachungaji wa muda ambao hufanya kazi zingine wakati wa wiki, na huwatembelea watu wakati wa jumamosi na kuhubiri wakati wa Jumapili.


"Makanisa ya eneo moja yanapoungana pamoja huwa yameunda "Jumuiya ndogo." Jumuiya ndogo hukutana mara tatu au mara nne kwa mwaka. Makanisa yetu ya

jumuiya ndogo yaliungana pamoja mwaka uliopita na yakaanzisha shughuli maalum. Pengine unaweza kumkumbuka mchungaji Mapoma ambaye alikuwa mgeni wa heshima.

"Kanisa letu pia ni sehemu ya "Jumuiya Kuu ya Wabatisti". Jumuiya Kuu imeundwa na makanisa yote ya Kibatisti yaliko nchini kote. Huwa tunatuma pesa kila mwezi kwa ofisi ya Jumuiya Kuu iliyoko katika mji wetu mkuu. Jumuiya Kuu hukutana mara moja kwa mwaka wakati ambapo sisi huamua tutakavyotumia pesa zilizotolewa. Njia mojawapo ambayo pesa hizi hutumiwa ni kwa kuwasaidia wamisheni kumi ambao huenda katika kila sehemu ya nchi yetu wakihubiri Injili."

"Asante sana mchungaji," Patrick akasema. "Sasa najua jinsi niwezavyo kushiriki pamoja. Kwani ninapotoa na kuomba na kushuhudia pale nilipo, huwa nasaidia ili Kristo ahubiriwe ulimwenguni kwote."

"Patrick, ilikuwa vizuri kuzungu-mzana nawe," mchungaji aka-mwambia, "Nimefurahi kwa sababu mahubiri yangu yalikufanya ufikirie jinsi uwezavyo kuwa mmisheni pale ulipo."



## KAZI YA KUFANYA

Andika hapo chini baadhi ya kazi ambazo zinaweza kufanywa na waamini wa sasa kwa kutimiza Agizo Kuu la Kristo.

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_

Piga mstari chini ya orodha ya maneno yafuatayo ambayo yanaeleza itikio la Wakristo kwa ulimwengu:

mwenye kuomba kumtoaaji

|           |                 |
|-----------|-----------------|
| kushiriki | msema kweli     |
| mchoyo    | mwenye kuhusika |
| mpweke    | mkatili         |
| kuhusika  | mpole           |
| kupenda   | kutojali        |

mwenye upendo

kufikiria nafsi yake

mwenye kumcha Mungu

mwenye kuhurumia

Piga mstari kutoka mwanzo wa sentensi hadi kwa sehemu ya pili ambayo itakamilika vyema sentensi hiyo.

Makanisa ya nchi Jumuiya ndogo.  
moja huungana  
pamoja ili kuunda

Mathayo 28:18-20  
inajulikana kama Jumuiya kuu.

Kundi la makanisa Agizo kuu.  
la sehemu fulani  
huungana pamoja ili  
kuunda

Jibu maswali yafuatayo yanayohusu jumuiya ya kanisa lako.

1. Jina la jumuiya ndoyo ni \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
2. Kiongozi wetu wa jumuiya ndogo ni \_\_\_\_\_
3. Mwaka uliopita kanisa letu lilitoa Sh. \_\_\_\_\_ kwa jumuiya ndogo na Sh. \_\_\_\_\_ kwa jumuiya kuu.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yale niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari” (Mathayo 28:19-20).

1. Je! ni amri zipi tatu ambazo Yesu aliwaamuru wafuasi wake? \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
2. Je! Yesu aliwaahidi nini wafuasi wake? \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_



## **VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA**

### **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

### **SURA YA KUMI NA MOJA**

## **UWAKILI WA MAISHA**

**MASOMO YA BIBLIA:** Malaki 3:10;  
1 Wakorintho 6:19-20, 16:2

**Je! wakili ni nani? Wakili ni yule** mtu ambaye anasimamia mali ya mtu mwingine. Kuna mawakili hotelini, katika ndege na hata melini. Huwashughulikia wageni, chakula chao na kutunza mizigo yao.



Sisi ni mawakili kwa sababu tunatunza vitu ambavyo Mungu ametupatia: maisha, vipawa, wakati, karama za Roho na mali.

**Vyote ni mali ya Mungu.** Mungu aliumba kila kitu, na vyote tulivyonavyo huja kwetu kama zawadi kutoka kwa Mungu. Biblia inasema kwamba Mungu atatuuliza siku moja tueleze jinsi tulivyotunza na kutumia vitu alivyumba na akatupatia.

**Sisi ni mawakili wa Mungu. Je!** tuliwezaje kuwa mawakili wa mali ya Mungu? Hii ilianza katika Bustani ya Edeni.

Mungu alimwumba mwanadamu baada ya kuumba ulimwengu, na vyote vilivyomo. Mungu akasema, "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, ...wakatawale...kila chenye kutambaa... juu ya nchi." (Mwanzo 1:26) Kutawala inamaanisha kuwa na wajibu, au kuwa wakili wa muumbo wa Mungu.

**Mawakili wa pesa zetu.** Malaki 3:10a inafundisha kuhusu uwakili wa pesa. Inasema kwamba, "Leteni zaka



kamili ghalani.” Mwakili wazuri watatoa zaka ya malipo yao katika nyumba ya Mungu.

Pengine hutakuwa na pesa nyingi za kutoa zaka wakati ungalipo shuleni. Hali unaweza kuwa mwaminifu kwa kutoa zaka na kile kidogo ulichonacho. Itakuwa rahisi kwako kutoa zaka kubwa wakati upatapo pesa nyingi.

Watu hawakuwa na pesa za kutoa katika nyumba ya Mungu wakati Agano la Kale lilipoandikwa. Hata hivyo, walileta sehemu ya kumi ya mali waliyokuwa nayo. Wakati mwingine walitoa mazao waliyovuna au nafaka. Walimtolea Mungu sehemu ya kumi ya vile waliyokuwa navyo.



Mtume Paulo ameandika katika Agano Jipya kwamba tunapaswa kutoa zaka zetu katika nyumba ya

Mungu siku ya kwanza ya wiki. Twasoma katika 1 Wakorintho 16:2 kwamba, “Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadri ya kufanikiwa kwake, ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja.”

Kifungu hiki kinafundisha mambo matatu:


1. Tunapaswa kutoa kwa utaratibu. (Kila siku ya kwanza ya juma.)
2. Kila mmoja anapaswa kutoa. (Kila mmoja wenu anapaswa kuweka akiba.)
3. Tunatoa kulingana na kile tulicho nacho. (Jinsi anavyofanikiwa)

**Mwakili wa wakati (muda) wetu.**  
Sote hatuna pesa kiwango kimoja. Hata hivyo sote tuna muda iliosawa sote. Tuna masaa ishirini na manne kila siku na siku saba kwa wiki. Sote



tunaweza kuamua kuwa mawakili wema au mawakili wabaya wa wakati wetu.

Lilly ni wakili mzuri wa wakati wake. Humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani, kubeba kuni na kuipikia jamaa chakula. Hufanya



vizuri kazi yake ya shule na humpelekea mwalimu kazi aliyofanya wakati ufao. Huamka asubuhi na mapema ili kuwa na muda wa kusoma Biblia yake kabla ya kuanza kazi. Hutumia vyema wakati wake.

Rafikiye Lilly aitwaye Elizabeth huacha kufanya kazi aliyopewa shuleni na huwa hayuko tayari kumjibu mwalimu amwulizapo swali akiwa darasani. Huwa analalamika wakati mamake anapomwambia amsaidie na kazi za nyumbani. Hutumia muda mwingi akiwatembelea rafiki zake, lakini hawi na muda wa kushiriki na Mungu kila siku. Elizabeth si wakili mwema wa wakati wake.

Tunapopanga kuwa na wakati wa kushiriki na Mungu kila siku, yeye hutuongoza katika kutumia vyema wakati wetu uliobakia.

**Wakili wa miili yetu.** Mungu alitupa uzima, na tunapaswa kumshukuru kila siku kwa sababu tuko hai. Mtume Paulo aliandika kuhusu umilikaji wa Mungu wa miili yote katika 1 Wakorintho 6:19-20. Alisema kwamba, "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu

aliye ndani yenu, aliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe, maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu."



Tunapaswa kuitunza miili yetu ili iwe na afya nzuri, na kutofikiria mambo maovu. Jinsi tutunzavyo miili yetu huwa ni ushuhuda wa ushirika wetu na Mungu. Je! wewe ni wakili mwema wa mwili uliopewa na Mungu? Je! mwili wako unafaa kama mahali pa kuishi pa Roho Mtakatifu wa Mungu?

**Mawakili wa vipawa vyetu.** Mungu amempa kila mmoja wetu kipawa fulani. Watu wawili hawawezi kuwa na kipawa kimoja, kwani sote tu tofauti. Mungu anatutaka tutumie vipawa alivyotupa kwa utukufu wake.

Baadhi ya vipawa au uwezo ambao watu wanao ni: kipawa cha uimbaji, kucheza gitaa, kufundisha, kufanya

urafiki, kucheza mpira, kushona, kufanya kazi na mashine, na kadhalika. Andika katika nafasi ifuatayo baadhi ya vipawa uliopewa na Mungu.

---

---

---

---

---

### KAZI YA KUFANYA

Andika herufi ya K (kosa) kando ya sentensi ambayo si ya kweli, na herufi ya S (sawa) kando ya sentensi ambazo ni za kweli.

—Watu wazima tu ndio wanao paswa kuwa mawakili.

—Ni lazima mtu awe tajiri ndipo awe wakili mwema.

—Sisi ni mawakili wa miili yetu.

—Mawakili hutunza tu pesa walizonazo.

—Maskini hawezi kuwa wakili.

Andika vizuri herufi zifuatazo ili ugundue yale ambayo sisi ni mawakili wake.

### TIWAKA PEAS PIAVWA ILIMI

---

---

Chora mviringo kwenye maneno ambayo yatakamilisha vyema sentensi hii:

Wakili ni mtu ambaye anamwibia mtajiri wake.

mtu ambaye anafanya kazi ya usafi wa nyumbani ili alipwe.

mtu ambaye anasimamia mali ya mtu mwingine.

### KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa"** (Mathayo 6:33).

Je! ni nini cha muhimu zaidi maishani mwako? Je! ni mtu, kitu ulichonacho, tamaa ya kwenda shuleni, umbo lako, au kitu kingine? Andika katika nafasi ifuatayo mtu, kitu ulichonacho, au kile unacho-kifikiria sana kila wakati.

---

Andika **amri** iliyoko katika kifungu cha kukumbuka.

---

Andika **ahadi** iliyoko katika kifungu cha kukumbuka.

---

Mtakuwa mawakili wema iwapo mtamtafuta kwanza Kristo na ufalme wake maishani mwenu.

Andika katika nafasi ifuatayo jinsi utakavyokuwa wakili mwema wa mwili wako, wakati, pesa au vipawa wiki hii.

---

---

---



# **VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

## **MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**

### **TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

## **SURA YA KUMI NA MBILI**

### **MWABUDU MUNGU**

**MASOMO YA BIBLIA: Luka 4:16-22**

Jane alimwuliza mamake wakati wa Jumapili asubuhi walipokuwa wakirudi nyumbani kutoka kanisani kwamba, "Mama, kwa nini tunaenda kanisani?"

Mamake alisimama na aka-mwangalia. Akamwambia huku akitabasamu, "Tunaenda kanisani kwa sababu tunampenda Mungu na tunataka kumwabudu."

Jane hakutosheka na jibu hili la mamake. "Lakini mama, kwa nini hasa tunaenda kanisani kuabudu?" Jane akauliza. "Kwa nini tusi-mwabudu tukiwa nyumbani, au shambani kwetu, au tunapotembea uwanjani?"


"Tunaweza kumwabudu Mungu popote tulipo," mamake akamjibu. "Tunaweza kumwabudu tunapoosha vyombo, tunapofanya kazi shambani, tunapotembea barabarani, tunapochunga mifugo au tunapoteka maji mtoni."

"Hata ingawa tunaweza kumwabudu tukiwa mahali pote," mamake akaendelea. "Yeye Mungu ana mahali maalum ambapo tunaweza kumwabudia. Ametupatia nyumba yake, yaani kanisa. Hapo ndipo tuwezapo kukutana na wengine ambao wanataka pia kumwabudu."

Jane alikuwa yungali na maswali, "Bado sijaelewa," Jane akasema. "Kwa nini jengo la kanisa liwe ndipo mahali maalum pa kufanyia ibada?"

Mamake aliendelea kumwelezea, "Mungu aliwaambia wafuasi wake kukutana pamoja katika nyumba yake kuimba, kuomba, kusikiliza neno lake na kumsifu.


"Twasoma katika Agano la Kale kuhusu maskani matakatifu, mahali pa kwanza ambapo Bwana aliwatolea watu wake ili waweze kufanyia ibada. Lilikuwa tu hema, lakini Mungu alikuwa na mpango jinsi watu wake watakutana naye. Mungu alitoa maelezo maalum jinsi ya kujenga



maskani matakatifu, yule ambaye alitakiwa kutoa dhabihu, kuwasha mishumaa na kutoa sadaka. Watu waliheshimu sana wakati huu wa ibada.

“Je! Yesu alimwabudu Mungu?” Jane akauliza. “Ndiyo,” mamake alimjibu. “Hii ndiyo sababu nyingine tunajua kwamba Mungu anatataka tumwabudu tukiwa katika nyumba yake. Jane, wakati Yesu alipozaliwa, watu wa Mungu hawakuwa wakifanyia ibada katika hema. Hekalu kubwa lilikuwa limejengwa pale Yerusalemu wakati wa utawala wa Mfalme Sulemani.”

“Je! Yesu aliabudu pale?” Jane akauliza.



“Alienda kuabudu Yerusalemu mara moja kwa mwaka. Nafikiri unakumbuka hadithi ihusuyo wakati alipoenda kuabudu huko na wazazi wake kwa mara ya kwanza. Walimtafuta sana.”

“Nafahamu kilichofanyika,” Jane akamkatiza. “Alikuwa akizungumza na waalimu wakubwa Hekaluni, na hapo ndipo walipompata.”


“Hiyo ni kweli kabisa. Usisahau sababu iliyowafanya kwenda Yerusalemu, walitaka kumwabudu Mungu wakiwa hekaluni.”

“Hekalu la Yerusalemu hapakuwa ndipo mahali pa pekee pa kuabudia. Kulikuwa na sinagogi mahali po pote ambapo palikuwa na jamaa wapatao kumi wa Kiyahudi.”

“Je! masinagogi yalikuwa makubwa kama Hekalu?” Jane akauliza. “La,” mamake akamjibu, “Lakini palikuwa mahali ambapo watu walienda kufanyia ibada kila siku ya Sabato.”

Jane na mamake walienda hadi kwa barazani kwao. Walikaa chini halafu mamake akadokezea, “Kwa nini usijisomee mwenyewe kutoka kwa Biblia yako? Fungua katika Injili ya Luka sura ya nne na usome kuanzia kifungu cha kumi na sita hadi ishirini na moja.”

Jane alisoma vifungu hivi na akamgeukia mamake na kusema, "Kwa hivyo alienda katika sinagogi lililokuwa karibu na kwao pale Nazareti." "Ndiyo, Jane," mamake akaendelea. "Utaona kwamba ilikuwa desturi yake kwenda katika sinagogi wakati wa sabato.



"Yesu alimwabudu Mungu popote alipokwenda. Maandiko mengi yanatwambia kwamba alikutana na waamini wengine alipoenda kuabudu katika sinagogi wakati alipokuwa akitembelea sehemu mbali mbali pale kwao," mamake akamwelezea.

"Sikufikiri kwamba Yesu alitakiwa kuabudu kwa kuwa alikuwa Mwana wa Mungu," Jane akawaza.

Mamake alisimama, akamshika mkono na akasema. "Yesu alijisikia kuwa karibu na Baba yake alipoabudu na wengine, nasi pia hujisikia hivyo. Hii ndiyo sababu tunaenda kanisani mwetu kila Jumapili. Mungu hufurahia tunapomwabudu tukiwa pamoja.

"Jane, njoo," mamake akamwambia, "Baba yako atakuwa na njaa atakapofika nyumbani. Tunatakiwa kupika haraka."

## KAZI YA KUFANYA

Weka alama (✓) kwenye jibu lililo la kweli.

Yesu alienda mara kwa mara kuabudu:

\_\_\_\_katika sinagogi.

\_\_\_\_shambani.

\_\_\_\_katika soko la Nazareti.

Jaza nafasi zilizoachwa: Maandiko yenyewe ni ya Luka 4:16a.

"\_\_\_\_\_Nazareti, hapo alipo-lelewa, na siku ya sabato akaingia katika \_\_\_\_\_kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome."

Chora mviringo juu ya njia ambazo ninyi hutumia kwa kuabudu katika kanisa lako:

kuzungumza na rafiki

kusoma Biblia

kusikiliza mahubiri

kuomba

kuimba nyimbo

kuandika

kutoa sadaka

kula peremende

Chora picha ya kanisa lako katika nafasi ifuatayo:

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Wala sisi hatutaiacha nyumba ya Mungu wetu" (Nehemia 10:39b).**

Tunapaswa kumwabudu Mungu kwa sababu yeye yu mtakatifu na kwa sababu tunampenda. Hatuna mahali pazuri ambapo tunaweza kumwabudia Mungu isipokuwa katika nyumba yake, yaani kanisa. Tuendapo kanisani hutarajia kusikia uwepo wake pamoja nasi.

Andika baadhi ya sababu ambazo zitakufanya kutoiacha nyumba ya Mungu, katika nafasi ifuatayo:

---


---

---

---

---

Picha ifuatayo inaonekana kama kioo cha dirisha kimechafuliwa kwa michoro. Andika katika kila sehemu ya kioo njia moja ambayo ninyi humwabudia Mungu katika kanisa lenu. Utapaswa kuchora kwa rangi kila sehemu iwapo mna kalamu za rangi (Crayons).





**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**  
**MWAKA WA TATU      KITABU CHA TATU**  
**TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA**

**J3 - 3Ps**

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All rights reserved

**SURA YA KUMI NA TATU**  
**KUHESHIMU NYUMBA YA MUNGU**

**MASOMO YA BIBLIA:** Zaburi  
122:1; 46:10; 51:1-2; 100

Julius alienda nyumbani kwa rafikiye Ayubu, Jumapili moja wakati wa asubuhi. Akamwambia, "Ayubu, naenda kanisani, njoo twende pamoja." Wazazi wa Ayubu walikuwa Waislamu, lakini hawakwenda msikitini mara kwa mara. Hata

mwaka ulikuwa umepita tangu walipoenda kuabudu humo.

Ayubu alifikiria kidogo halafu akasema, "Haya, naweza kwenda, sina kazi ya kufanya leo." "Vyema," Julius akaongezea, "Ningejua ningekwalika mapema." Ayubu alibadilisha shati lake na wote wawili wakaanza kwenda kanisani.



Walipofika huko Ayubu alimwambia, "Utaniambia jinsi ya kutenda, hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuhudhuria kanisani."

"Kweli," Julius akasema, "Nadhani utafurahia. Kwanza kabisa tuta-hudhuria masomo ya Biblia, halafu twende kwa ibada kanisani." Julius alimjulisha Ayubu kwa marafiki zake kabla ya mwalimu kuanza kufundisha. Wote waliohudhuria walikuwa karibu wa umri mmoja, naye Ayubu aliweza kuwatambua baadhi yao ambao walikuwa wakisoma katika shule moja.

Ayubu alikaa tuli na kuwaangalia wakati washiriki nao waliposoma Biblia, na kuomba, na kujibu maswali, na kukariri vifungu vya Biblia hali wakijadiliana somo hilo.

Kabla ya kuondoka, mwalimu aliwahimiza kuwa na heshima wanapoenda kanisani. Akawaambia, "Mara kwa mara huwa tunasahau kwamba ni nyumba ya Mungu, na tunatakiwa kuonyesha heshima kwa kuwa watulivu."

Walipokuwa wakitoka darasani Ayubu akasema, "Je, mnajua je mengi kuhusu Biblia? Sijawahi kusikia lo lote kati ya yale mliyozungumzia." "Utaelewa kwa haraka iwapo utakuja nami wakati nijapo," Julius akamwelezea. "Nimekuwa nikija kanisani tangu nilipokuwa mdogo na ndiyo sababu ninayafahamu haya yote."

Julius alimwongoza rafiki yake hadi mlangoni wa kanisa na wakaingia na kukaa kiti cha pili kutoka mbele. Kwaya iliingia mara moja kupitia

mlango wa nyumba ikiwa inaimba wimbo usemao, "Hii ndiyo siku aliyoiumba Bwana, nitaifurahia na kuisherehekea." Umati wa walio-hudhuria walianza kuimba pamoja nao.

Ayubu aliona jinsi watu wale walivyoonekana wenye furaha. Alikuwa akifikiria kwamba wakati huu ungekuwa wa kukaa tu na kutulia. Hakutarajia kwamba kungekuwa na furaha kama hii.

Mchungaji Bulus aliwaambia washiriki wasimame na kuimba kutoka kwa kitabu cha nyimbo. Halafu akaomba.

Ayubu alimgeukia Julius na akamwong'onezea, "Je! alisoma ombi lile?" "La," Julius akatikisa kichwa chake. "Huwa hatusomi maombi katika kanisa letu. Ombi hili lilitoka tu rohani mwa mchungaji."

Waliendelea kuimba, naye shemasi akasoma Maandiko Matakatifu. Kwaya iliimba huku wakitoa sadaka. Ayubu hakuwa amewahi kuhudhuria ibada kama hii. Akajiwazia, "Nitamwuliza Julius kile wanachofanyia sadaka baada ya ibada."



Mchungaji Bulus alisimama tena ili kusoma Maandiko ya Biblia. Alisoma vifungu tofauti vya Zaburi, ambavyo aliviita vitabu vya nyimbo vya Biblia.

Mchungaji Bulus alihubiri juu ya "Kuabudu katika Nyumba ya Mungu." Alisema kwamba anawataka watu wake:

1. Wafurahi wanapoingia katika nyumba ya Mungu.
2. Watambue uwepo wa Mungu katika nyumba yake.
3. Wawe tayari kutubu dhambi yoyote iliyoko maishani mwao.
4. Wawe tayari kumtumikia Mungu mahali po pote.
5. Wajazwe na sifa na shukrani, kwa sababu Mungu ni mwema.

Ayubu alifikiria kwamba angechoka sana akiwa anasikiliza mahubiri, lakini muda ulipita haraka sana. Mahubiri yake yalieleweka kwa urahisi. Ayubu aligundua kwamba rafiki yake, Julius, alikuwa akiandika yale ambayo alihubiri.

Kwaya aliimba tena, na kukawa na maombi mengine kabla ya mwisho wa ibada. Watu walitoka nje kwa heshima.

Julius akamwambia Ayubu kwenda kumsalimia mchungaji wake. Walipoufikia mlango Julius akasema, "Mchungaji Bulus, huyu ni rafiki yangu, Ayubu. Hii ndiyo mara yake ya kwanza kuhudhuria kanisa letu, na nilijua kwamba ungetaka kukutana naye." Walisalamiana na mchungaji akamkaribisha.

"Asante sana Julius, kwa kuleta rafiki," Mchungaji akamwambia. "Tunaweza kukutana wiki hii na unipeleke kwa akina Ayubu ili tufahamiane vizuri."

"Je! unafikiri mchungaji atanitembelea?" Ayubu akauliza walipokuwa wanaelekea nyumbani.

"Ndiyo," Julius akamjibu, "Yeye huwatembelea wageni wote wanaofika kanisani kwetu. Hata hivyo, nitamweleza na kumkumbusha."

"Je! tunaweza kuzungumza kwa dakika chache kabla ya kwenda nyumbani?" Ayubu akasema. "Mchungaji alisema mambo fulani katika mahubiri yake ambayo sikuelewa. Nilikuona ukiandika, kwa hivyo nafikiri unaweza kunisaidia."



“Ninayo hapa,” Julius akamwambia, “Hebu tukae hapa kivulini na nitajaribu kukuelezea cho chote ambacho hukuelewa.”

Vijana hawa waliongea sana hadi saa tisa mchana, kabla ya kuagana. Walianza kuwa marafiki wakubwa, naye Julius aliweza kumjulisha Ayubu kwa rafiki yake mkubwa aitwaye Yesu.

### KAZI YA KUFANYA

Kata kwa mstari maneno yaliyo na kosa katika sentensi zifuatazo;

1. Tunapoingia katika nyumba ya Mungu tunapaswa (kuzungumza na rafiki zetu, kuzungumza na Mungu).
2. Ni lazima (tumsikilize mhubiri, tuwasikilize rafiki zetu) tuwapo katika nyumba ya Mungu.
3. Tunapaswa kutoa (zaka na sadaka, mbwa, na viatu vichafu) tuwapo kanisani.
4. Mchungaji hutupa (mafundisho yake, ujumbe wa Mungu).
5. Tunapaswa (kutunza, kuharibu) viti na jengo la kanisa.

Weka alama (✓) kwenye jibu lililosawa.

Je! Mungu anatumia tufanyaje tuendapo katika nyumba yake?

\_\_\_\_\_tulale \_\_\_\_\_tuzungumze na rafiki zetu \_\_\_\_\_tumsifu kwa nyimbo.

Hapo chini kuna Zaburi 100. Chora mviringo kwenye maneno yafuatayo:

mfanyieni Bwana shangwe, mtumikieni, njoni, jueni, ingieni, mshukuruni, lihimidini jina lake.

Mnapaswa kufahamu kwamba maneno haya ni amri au vitendo ambavyo tunapaswa kufanya mioyoni mwetu.

Mfanyieni Bwana shangwe dunia yote, Mtumikieni Bwana kwa furaha; Njoni mbele zake kwa kuimba; Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake.

Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru;

Nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini jina lake;

Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele; Na uaminifu wake vizazi na vizazi.

Zaburi 100 ni moja wapo ya Maandiko ya kupendeza sana ya Biblia. Jaribu kuyakariri ili uyatumia kumsifu Bwana wakati unapomwabudu.

### KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu” (Zaburi 46:10).

Ni vigumu sana kutulia. Mara kwa mara huwa tunataka kufanya jambo fulani, kwenda huku na huko, au kusikiliza muziki. Mungu anataka tumsikilize na tuwe watulivu ili tusikie vyema.

Andika kwenye mstari ufuatao wakati ambapo utakubaliana kuwa peke yako na Mungu, ili umfahamu vyema.

---

---

---